epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumanne Oktoba 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581816
www.ippmedia.com
MWANGA W
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

UKURASA WA 3
**CCM** yakemea siasa za ukabila, udini na ukanda

UKURASA WA 4
**Uboreshaji** wa daftari wapigakura waiva Zanzibar




UKURASA WA 5
**Shilingi** 200 ilivyokatisha uhai wa dereva kwenye kamari



UKURASA 21
**TEN HAG ALIA NA WACHEZAJI WAKE MAN UTD**



# Warioba asimulia jinsi alivyotaka kujiuzulu uwaziri

• **Kisa** kutofautiana na Sokoine, Samia asisitiza uadilifu, watu kuacha tamaa ya vyeo... *Endelea ukurasa 2*



**Mtaalamu aeleza namna ya kutambua dalili tatizo afya ya akili mahali pa kazi**
UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan akibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi wa kitabu kuhusu Maisha na Uongozi wa Hayati Edward Moringe Sokoine, aliyekuwa Waziri Mkuu mwaka 1977 mpaka 1980 na 1983 hadi 1984, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Balozi Joseph Sokoine, mtoto wa Hayati Sokoine. **PICHA: IKULU**

## Waliombaka 'binti wa Dovya' jela maisha
UK.3

**MICHEZO** **FADLU AFURAHIA UKOMAVU WACHEZAJI WAKE** UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Warioba asimulia alivyotaka kujiuzulu uwaziri wa sheria

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI Mkuu na Makamu wa Kwanza Rais Mstaafu, Jaji Joseph Warioba, amesimulia alivyotaka kujiuzulu nafasi ya Waziri wa Sheria, wakati hayati Edward Sokoine alipokuwa Waziri Mkuu, kutokana na kutoridhika na uamuzi wa kutaka kubadili sheria.

Wakati huo, Warioba alikuwa pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa uongozi wa Awamu ya Kwanza chini ya Mwalimu Julius Nyerere kabla ya kuwa Waziri Mkuu na makamu wa kwanza wa Rais mwaka 1985 hadi 1990 wakati wa serikali ya awamu ya pili iliyoongozwa na Alhaj Ali Hassan Mwinyi.

Jaji Warioba alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kitabu cha 'Edward Moringe Sokoine: Maisha na Uongozi Wake', uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, jijini Dar es Salaam.


Warioba katika simulizi hiyo, alitumia dakika 19 kueleza nyakati ngumu na nzuri walizofanya kazi pamoja na Sokoine, huku akimwelezea alikuwa mtu wa aina gani na umuhimu wa kitabu cha maisha ya kiongozi huyo kwa viongozi wa Kitanzania, hususani vijana.

Alisema Sokoine alichukia sana wala rushwa na wahujumu uchumi, hivyo alipoteuliwa kuwa Waziri Mkuu kwa mara ya pili (1983 hadi 1984 alipofariki dunia), alipendekeza mabadiliko ya sheria ili kupambana na watu waliojihusisha na mambo hayo.

Kwa mujibu wa Jaji Warioba, katika mabadiliko hayo, Sokoine alipendekeza kesi za uhujumu uchumi ziwe na mahakama zake maalum, zisikilizwe faragha, hata maneno ya kusikia kuhusu wahujumu uchumi yakubalike.

Alisema binafsi hakukubaliana na hayo kwa sababu mbalimbali ambazo alisema alizitoa kwenye Baraza la Mawaziri na mbele ya Rais Nyerere.

Jaji Warioba ambaye amewahi kuwa Jaji wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, alisema pamoja na kutoa sababu za kupinga vipengele hivyo, hakukubaliwa kwa sababu aliyepinga alikuwa peke yake, hivyo alikubaliana na matokeo. Hata hivyo, alisema alitangaza kujiuzulu kwa sababu hakuwa tayari kusimamia vipengele hivyo akiwa waziri wenye dhamana.




"Sokoine hakupenda hilo, akaniita, akasema wewe umekuwa mstari wa mbele kupambana na rushwa. Sasa kwa kitu kidogo kama hiki unasema unaacha kazi? Nikamwabia hapana Waziri Mkuu, hili ni la muhimu zaidi," alisimulia.

Jaji Warioba ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Tanzania mwaka 2012, alisema alimweleza sababu ya kujiuzulu kuwa aliamini kama utekelezaji wa sheria hiyo ungeanza ungesababisha madhara makubwa kwa kuwa inavunja misingi ya utawala bora na kuingilia haki za binadamu.

Baada ya kumpa sababu hizo, alisema Sokoine alimpeleka kwa Nyerere ambaye aliwashauri wakaondoe vipengele vya kesi kusikilizwa faragha, lakini vipengele vya utaratibu maalum na kutoruhusiwa dhamana vibaki.

Alisema baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Nyerere, Sokoine alimwelekeza kufanya marekebisho na kesho yake ampelekee kwa ajili ya kuendelea na utaratibu, na kwamba alitekeleza na sheria ilipita Aprili, 1983.

Baada ya sheria hiyo kuanzia kutumika, alisema mambo yale yale aliyohofia kuwa yangetokea, yaliyotokea kwa sababu watu walikamatwa kwa utaratibu usio nzuri, mali kukamatwa na malalamiko ya wananchi kuwa mengi.

Alisema malalamiko yalizidi na ilitokea baada ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kanda ya Ziwa kukamatwa kwa tuhuma za uhujumu uchumi, ndipo wazee walikwenda kumwona Nyerere ambaye aliandika ujumbe maalum kutoa maelekezo kwa Sokoine kutoa dhamana.

Alisema Sokoine akamwandikia yeye (Warioba) barua ya kumwomba amwachie na yeye akakataa kwa kuwa sheria hairuhusu.

"Alipiga simu yeye mwenyewe (Sokoine) kuniita ofisini kwake. Nilipofika kabla sijaingia, akasema Joseph wewe ni mtu wa aina gani? Rais anatoa amri, wewe unasema hutekelezi? Basi na mimi kwa kuwa tulikuwa tunataniana nikacheka tu.

"Nikasema si uliniburuza ukanipeleka Msasani (Kwa Nyerere) na ulisikia mkuu alisema nini? Kwamba dhamana isitolewe? Na Rais alisema msivunje sheria hata ikiwa mbaya bali muibadili," alisimulia Warioba.

Alisema baada ya mazungumzo hayo, Sokoine alimwelewa lakini alisema hawawezi kwenda kumwambia mkuu wa nchi kuwa haiwezekani bali waichukue kama maagizo ya kubadili sheria, hivyo alimwagiza kufanya mabadiliko ya sheria na alifanya hivyo na kuipeleka bungeni Juni, 1983 hivyo ilidumu kwa miezi miwili tu.

Pamoja na yote, alisema Sokoine alikuwa kiongozi mwadilifu na mchapakazi, aliyependa kuuliza maswali mengi kuhusu utendaji kazi wa watumishi pia alitoa nafasi ya kuulizwa maswali.

"Akiwa amezungukwa na Baraza la Mawaziri Vijana, Sokoine alikubali kukosolewa na ikitokea amepishana lugha na kiongozi mwenziwe, hakuwa mtu wa kuweka kinyongo. Alihakikisha wanamaliza tofauti na waliendelea na kazi kama kawaida," alisema.

Pia alisema kiongozi huyo alikuwa anathamini mambo ya kimila hasa uongozi, akitolea mfano kipindi CCM inaanza kutengeneza kanuni za mgombea urais, alipinga mpango wa kuchaguliwa kwa kura za karatasi na kushauri wachaguliwe kwa kuangaliwa viongozi wanaowajua kwa utendaji kazi wao.

Alisema kiongozi huyo alikuwa akijifunza kwa watu wa kawaida na aliishi maisha ya kawaida ndani ya nyumba za kimasai (maboma) hata kila anapokuwa nyumbani kwake, wanakijiji walikuwa wakikusanyika na kumweleza shida zao.

# Samia ahimiza viongozi uaminifu, nidhamu

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewakumbusha viongozi kuiga mfano wa aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Sokoine, kwa kufanya kazi kwa uaminifu, nidhamu na uchapakazi. Amesema wakifanya hivyo vyeo vitawafuata badala ya kuvikimbilia.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika hafla ya uzinduzi wa kitabu cha kiongozi huyo cha 'Edward Moringe Sokoine, Maisha na Uongozi Wake'. Rais Samia alisema viongozi wakifanya kazi kwa bidii na uaminifu, hawatokuwa na haja ya kukimbizana na vyeo bali vitawafuata kulingana na matokeo ya utendaji kazi wao.

"Katika hili tunajifunza kwamba ukiwa mwadilifu na mchapakazi, huna haja ya kukimbizana na vyeo bali vyeo vitakufuata ulipo," alisema.

Alisema Sokoine alikuwa mwaminifu kwa mamlaka yake ya uteuzi na wananchi ndiyo maana alipewa majukumu mengi katika umri mdogo, ikiwamo uwaziri mkuu.

Rais alisema kitabu hicho pia kinawafundisha yeye (Samia) na viongozi vijana kufanya mambo yatakayoacha alama kwa kuwa kiongozi huyo aliacha alama katika kila ngazi aliyoifanyia kazi kwa kusimamia vizuri miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa reli wa TAZARA.

Alisema alama nyingine aliyoiacha ni alikuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kushauri na ikapitishwa kuwa wanawake waandikishwe jeshini na mpaka sasa kuna viongozi wa nafasi za juu katika jeshi hilo.

### MAGEUZI YA KILIMO

Pia alisema Sokoine aliamini katika kilimo cha kisasa kupitia wataalamu, hivyo alisimamia uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ambacho mpaka sasa kinaishi maono yake ya kuzalisha wataalamu wengi wanaoendeleza sekta za kilimo na mifugo.

Alisema tangu kufariki dunia kiongozi huyo, serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwenye sekta ya kilimo kwa kuongeza bajeti kila mwaka hadi kufikia Sh. trilioni 1.25 kwa mwaka wa fedha 2024/25, iliyosaidia kuongeza maofisa ugani na kuwapatia vitendea kazi.

Ongezeko la bajeti, pia alisema limesaidia kuzalisha mbegu bora nchini, kutoa ruzuku kwa wakulima na kuongeza eneo la umwagiliaji hali iliyoongeza utoshelevu wa chakula hadi asilimia 128.

Alisema Sokoine alitaka viongozi wote wawe na mwelekeo mmoja na nia ya kulivusha taifa linapopitia wakati mgumu na kujiepusha kuanzisha sababu na vikwazo vya maendeleo bali wajikite kutafuta ufumbuzi wa matatizo.

Rais alisema kauli hiyo inaakisi mapito ya nchi hiyo katika vipindi mbalimbali kama vile mafuriko, hali ngumu ya uchumi, maradhi, vita na katika yote hayo viongozi wa nchi walitembea na maelekezo ya kiongozi huyo na hawakurudi nyuma hali inayosababisha uchumi kuwa himilivu.

"Nasema haya ili kuweka msisitizo kwetu kama viongozi kutokukwamishwa na changamoto zinazotukabili katika vipindi vigumu bali kutafuta njia mwafaka za kujikwamua na tuweze kusonga mbele," alisema.

Alisema kupitia kitabu hicho, nchi itajifunza ushahidi na maelezo mapya kuhusu mapito ya taifa ambapo serikali inapata uelewa wa kufanya uamuzi kulingana na hali ilivyo sasa.

Rais alisema kitabu hicho kinafundisha kuwa kiongozi si sababu ya kuacha malezi ya watoto kwa kuwa katika uongozi wake, Sokoine alikuwa baba na mlezi aliyesimamia nidhamu kwa watoto wake.

Alisema kiongozi huyo alisimama imara nchi ilipokumbwa na changamoto za kiuchumi, viwanda na afya na uhaba wa chakula, akiweka mkazo kuendeleza kilimo na kuruhusu biashara huria ili kukidhi mahitaji ya wananchi na kuboresha huduma.

Awali, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alimshukuru Rais Samia kwa kuridhia kuandikwa kwa tawasifu ya kiongozi huyo, kuidhinisha Sh. milioni 200 kwa ajili ya kukamilisha shughuli hiyo pamoja na kuandika dibaji ya kitabu hicho.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Paramagamba Kabudi, alisema kitabu hicho kinaelezea alama alizoziacha kiongozi huyo katika uongozi ikiwamo kuleta mapinduzi ya kilimo, kupambana na wahujumu uchumi, mageuzi ya elimu na utawala bora.

Alisema katika sura ya nne ya kitabu hicho inaeleza alivyopigania uwapo wa ofisi za bunge katika majimbo ambapo baada ya kula kiapo cha kuwa Mbunge wa Jimbo la Masai mwaka 1965 alihoji bunge ni lini ofisi za bunge zitajenga katika wilaya ambazo hazikupata ofisi ikiwamo ya Monduli.

"Katika nafasi hiyo ya ubunge wananchi wa Jimbo la Masai walimwona kuwa kiuongozi mwaminifu, mwadilifu, mkweli, asiyemlanguzi wa siasa," alisema.

Prof. Kabudi alisema kitabu hicho kinaelekezea mambo makubwa aliyoyafanya kiongozi huyo katika vipindi viwili walivyohudumu kama waziri mkuu ikiwamo kufanya kazi katika mazingira magumu.

Pia alisema Sokoine alikuwa mwanasiasa makini na mahiri aliyetetea kwa nguvu zake zote watu aliowaongoza hasa wanyonge, alikuwa mkweli na hakuogopa kusema na kutenda aliyoyaamini, alichukia uvivu na ubabaishaji katika maisha, hivyo alisimamia utekelezaji wa sheria, kupiga vita ubadhirifu wa mali za umma, wizi na uzembe.

HABARI KITAIFA

## ACT yaainisha haki wanazostahili kupata Watanzania

**Na Waandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo Taifa, Omar Ali Shehe, ametangaza rasmi haki za msingi wanazozipigania wananchi kupata huduma bora na kupata haki ya kikatiba ya kuishi.

Akihutubia wananchi wa chama hicho katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kiwanja cha Jongomeo Chambani, Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba, alisema chama hicho kinapigania hayo kwa kuwa ndio msingi wa maisha ya kila Mtanzania.

"Tunapigania haki ya kuchagua viongozi wanaotuongoza wakiwamo madiwani, wawakilishi, wabunge na Rais, tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi Wazanzibar tunateseka na kuongozwa na watu tusiowataka kuanzia majimbo hadi serikali," alisema.

Aidha, alisema Wazanzibar pia wanaopigania haki ya kuwa na Zanzibar yenye mamlaka kamili yenye kiti chake Umoja wa Mataifa na uwezo wa kujiamulia mambo yake yenyewe, ikiwamo uchumi na hakuna chama kingine chenye uwezo wa kupigania mamlaka kamili isipokuwa ACT-Wazalendo.

Alisema kuna vitendo vimeanza kufanyika vinavyokwenda kinyume na msingi ya demokrasia baada ya viongozi wa mitaa (masheha) kudaiwa na wananchi wamekuwa wakipita katika nyumba na kuchukua namba za vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi au za kadi za wapigakura bila ya kueleza malengo yake.

"Tumeshuhudia vitendo vinavyoendelea katika mkoa huu wa Mkoani masheha wanapita kila nyumba na kuchukua namba za vitambulisho vya wapigakura wakati serikali inapokuwa na jambo lazima itoe tangazo rasmi kitendo hicho kinachofanywa na masheha hakina nia njema," alidai.

# Waliombaka 'binti wa Dovya' jela maisha, faini milioni 1/-



Watuhumiwa wa kesi ya ubakaji na ulawiti kwa kundi wakitoka katika Mahakama Jumuishi ya Utoaji Haki Dodoma jana, baada ya kuhukumiwa kifungo cha maisha jela na kulipa faini ya Sh. milioni moja kwa kila mmoja. Hukumu hiyo ilitolewa jana na Mahakama ya Hakimu Mkoa wa Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**Paul Mabeja na Renatha Msungu,** DODOMA

WASHTAKIWA wanne wa kesi ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, Dar es Salaam, wamehukumiwa kifungo cha maisha na faini ya Sh. milioni moja kwa kila mmoja.

Washtakiwa hao walihukumiwa adhabu hiyo baada ya kukutwa na hatia na Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma.

Waliokumbwa na hukumu hiyo ni askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), mwenye namba MT (Mlinzi wa Taifa) 140105 Clinton Damas, maarufu kama Nyundo, Askari Magereza C.1693 Praygod Mushi, Nickson Jackson 'Machuche' na Amin Lema, anayejulikana pia kwa jina la Kindamba.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma, Zabibu Mpangule. Akizungumza nje ya mahakama, baada ya hukumu hiyo, Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Renatus Mkude, alisema kesi hiyo ilikuwa ikiendeshwa katika mahakama ya kificho (falagha) kutokana na aina ya makosa ili kulinda utu wa mwathirika.

Mkude alisema mahakama hiyo imewakuta watuhumiwa wote wanne na hatia baada ya upande wa Jamuhuri kuwasilisha mashahidi 18 na vielelezo 12 huku washtakiwa wakijitetea wenyewe.

"Kama tulivyowaomba wananchi wawe watulivu ili mahakama itoe hukumu na leo (jana) hukumu hiyo imetolewa baada ya washtakiwa kukutwa na hatia na kuhukumiwa kifungo cha maisha na kulipa faini ya Sh. milioni moja kila moja na adhabu zote zinaenda kwa pamoja," alisema Mkude.

Alisema kutokana na hukumu hiyo, upande ambao utakuwa haujaridhika, unaruhusiwa kukata rufani kwa ajili ya kutafuta haki.

Wakili wa Utetezi, Godfrey Wasonga, alisema wanaheshimu uamuzi wa mahakama lakini hawajaridhika na hukumu iliyotolewa kutokana na kasoro mbalimbali zilizokuwamo, ikiwamo nakala ya mashtaka (charge sheet).

Alisema walikuwa na shaka na uhalali wa nakala ya mashtaka kutokana kuwa na upungufu.

Wasonga alisema upungufu huo ni pamoja na wao kutokutajiwa eneo lililofanyika tukio lakini cha kushangaza hawajatajiwa muda wa vitendo hivyo vya kikatili vilivyofanyika.

Alisema inakuwaje binti alisema amewatambua washtakiwa hao, ilihali ilikuwa usiku na anadai alipigwa vibao na washtakiwa.

Pia alisema pia binti naye alipaswa kushtakiwa kwa sababu anasema alitongozwa na mtu mmoja aitwaye Kiboi na wakaelewa lakini cha kushangaza mtu huyo hajafikishwa mahakamani.

Alisema kosa hilo hata binti naye alipaswa kushtakiwa na kuendelea kusisitiza wateja wao bado wana nafasi ya kukata rufani ili kutafuta haki yao.

Kesi hiyo ilifikishwa katika mahakama hiyo Agosti 19, mwaka huu, na kuanza kusikilizwa mfululizo hadi jana ilipsomwa hukumu hiyo.

# CCM yakemea siasa za udini, ukanda na ukabila

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KATIBU wa Oganaizesheni wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Omar Ibrahim Kilupi, amekemea tabia ya baadhi ya wanasiasa waohamasisha udini, ukanda na ukabila.

Kutokana na kuwapo kwa wanasiasa hao, amewataka viongozi wa dini na wananchi kukemea tabia hizo .

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na waumini wa dini ya Kikiristo katika hafla ya kutimiza miaka 30 ya Kwaya ya Mtakatifu Michael Malaika Mkuu, Parokia ya Mpendae, Zanzibar.

Kilupi alisema viongozi wa dini nchini wanatakiwa kuelekeza nguvu zao katika kuhubiri na kutoa mafundisho ya kiimani ya kukemea kauli za uchochezi na ukabila zinazotolewa na baadhi ya wanasiasa kwa kuwa zinaweza kuingiza nchi katika machafuko.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wameasisi maridhiano ya kisiasa na kuruhusu utawala wa demokrasia, hivyo ni muhimu kwa kila mwananchi kuheshimu misingi hiyo.

Pamoja na maridhiano hayo, alisema kuna baadhi ya wanasiasa na wanaharakati wameanza kutoa kauli zinazoashiria uvunjifu wa sheria, ambazo zinatakiwa kupingwa na wananchi wote bila kujali tofauti zao za kisiasa na kidini.

Kilupi aliwasihi viongozi na waumini hao kuendeleza umoja, mshikamano na upendo wakati wote sambamba na kuiombea nchi iendelee kuwa na amani na utulivu.

"Wito wangu kwenu endeleeni kuwa wamoja. Msikubali kutumiwa na baadhi ya wanasiasa wanaohamasisha vurugu na kauli za kuwabeza viongozi wetu wakuu wa kitaifa kwani maendeleo yanayotekelezwa nyote mnayaona.

"Amani ndilo chimbuko la maendeleo haya tuliokuwa nayo hivi sasa hivyo tusikubali fursa hii ituponyoke kwa gharama yoyote," alisema Kilupi.

Kilupi alisema CCM imeendelea kusimamia sera zake kwa kuhakikisha serikali inatekeleza kikamilifu maendeleo kama ilivyoahidi katika kampeni za uchaguzi mkuu uliopita.

Pia aliwasisitiza waumini hao kutumia vizuri haki yao ya kidemokrasia kuhakikisha wanajiandikisha katika awamu ya pili ya daftari la kudumu la wapigakura ili wapate uhalali wa kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Naye Padri Antony Kanturu wa Parokia ya Mpendae, alisema kipaumbele cha kanisa hilo ni kutoa mahubiri yanayowaunganisha wananchi katika kuendeleza amani na upendo.

Katika risala yao, wanakwaya walisema kwa kipindi cha miaka 30 wamepata mafanikio mbalimbali yakiwamo kurekodi na kutengeneza albamu za nyimbo mbalimbali zinazoendelea kufanya vizuri katika soko la nyimbo za injili ndani na nje ya nchi.

Aidha walitaja changamoto zinazowakabili kuwa ni ukosefu wa gari ya kutoa huduma za usafiri na ukosefu wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya uandaaji wa nyimbo.

Kwaya hiyo ya Mtakatifu Michael Malaika Mkuu, ilianzishwa mwaka 1994 ikiwa na wanakwaya 15.




Balozi wa Tanzania Zambia, Luteni Jenerali, Mathew Mkingule (kulia), akiagana na Dk. Maiyer Msengi, baada ya timu ya madaktari wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kumaliza kambi ya matibabu ya moyo nchini humo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Uboreshaji daftari waiva Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

UBORESHAJI wa Daftari la Kudumu la Wapigakura Zanzibar, utafanyika kwa siku saba kuanzia Oktoba 7 hadi 13, mwaka huu, na vituo vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni.

Akifungua mkutano wa wadau wa uchaguzi kisiwani Pemba jana, Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Mbarouk Salim Mbarouk, alisema uboreshaji huo utajumuisha mikoa ya Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

Alisema uboreshaji huo ambao unafanyika kwenye mzunguko wa sita kwa mujibu wa kalenda ya tume kwa upande wa Zanzibar, utahusu Watanzania wote wanaoishi Zanzibar ambao wanastahili kuandikishwa kuwa wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Akizungumza wakati akifungua mkutano kama huo kisiwani Unguja, Mjumbe wa INEC ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Omar, aliongeza kuwa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024. Alisema tume itawaandikisha Watanzania waliopo Zanzibar ambao wametimiza umri wa miaka 18 na zaidi au watakaotimiza umri huo wakati au kabla ya tarehe ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Jaji Asina alisema Mtanzania huyo atakayeandikishwa ni lazima awe hajapoteza sifa kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi au sheria nyingine yeyote na awe anastahili kuandikishwa kuwa mpigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais.

"Kwa lugha nyepesi ni kwamba tume itamwandikisha Mtanzania yeyote aliyopo Zanzibar ambaye amekosa sifa za kuandikishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Hivyo, atakayeandikishwa kwenye Daftari la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi atapiga kura moja tu ya kumchagua Rais," alisema Jaji Asina.

Uzinduzi wa uboreshaji wa daftari ulifanyika Julai 20, mwaka huu, Kigoma na mpaka sasa umeshafanyika Tabora, Katavi, Geita, Kagera, Mwanza, Shinyanga, Mara, Simiyu, Manyara, Singida na sehemu ya mkoa wa Dodoma.

# Mtaalamu aeleza namna ya kutambua dalili tatizo afya akili mahali pa kazi

**Na Christina Mwakangale**

DALILI za tatizo la akili miongoni mwa wanajamii, hasa mahali pa kazi zinaweza kutambulika kirahisi, hivyo hatua kuchukuliwa haraka ili kumsaidia mwathirika na kumlinda dhidi ya vitendo hasi ikiwamo kujitoa uhai.

Aidha, imeelezwa kuwa afya ya akili ni ustawi kijamii, hivyo kuna umuhimu wa kuwapo utulivu wa kiakili mahali pa kazi na kupewa kipaumbele katika utoaji elimu namna ya kukabiliana na tatizo hilo. Muuguzi Mtaalamu wa Afya ya Akili kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Sofia Sanga, aliyasema hayo jana katika mada iliyohusu Umuhimu wa Kujali Afya ya Akili Mahali pa Kazi, kupitia mtandao iliyoandaliwa mwishoni mwa wiki na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNMH).

Kadhalika, alisema mahali pa kazi hutumia zaidi ya asilimia 50 ya saa 24 kwa siku, katika kazi rasmi au isiyo rasmi yenye lengo la kujipatia kipato, hivyo ni miongoni mwa maeneo ya chanzo cha ustawi duni wa akili, kutokana na ukosefu wa mbinu za kuzikabili.

Alisema kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), tafsiri ya afya akili imegawanyika sehemu tatu ambazo ni ustawi wa akili; uwezo wa akili binafsi wa binadamu kukabiliana na changamoto mbalimbali maishani; uwezo wa mtu kufanya kazi na kuzalisha; na uwezo wa mtu na mchango wake kwa jamii.

"Tunapozungumzia afya ya akili yaani ustawi wake ni mambo ya kawaida kabisa ambayo yako kwenye jamii. Kwa mfano ya kwanza ni changamoto ambazo ziko zaidi ya madeni mtu anadaiwa. Hii inatosha kabisa kumwathiri mtu asipojua namna ya kukabiliana nayo. Nataja madeni kwa sababu ni suala mtambuka.

"Aidha, deni la benki au mtu binafsi, au dukani kwa Mangi, unadaiwa mikopo ya Vicoba au rafiki yako hata kuna wengine walikula michango ya harusi ikageuka kuwa madeni. Huu ni mfano wa mtu ambaye ukahisi anapitia changamoto," alisema Sanga.

Aliiitaja changamoto ya pili kuwa ni kama vile kupoteza uhusiano, kazi, kuondokewa na mwenza, ndugu au jamaa. Alisema changamoto hizo zinaweza kupunguza uwezo wa afya ya akili ya mtu yeyote iwapo ustawi wake kiakili utayumbishwa.

Pia alisema viwango vya uwezo wa mtu kwa tafsiri ya pili ni jamii inavyompima katika ufanyaji kazi kama vile kuripoti kazini kwa muda uliopangwa, kutekeleza majukumu na kutoa matarajio kwa asilimia iliyowekwa.

"Mfano kazini mtu ambaye alitarajiwa afanye kitu hiki kulingana na majukumu yake na akaanza kufanya vitu vingine, ujue kuna kitu hakiko sawa kwenye afya yake kiakili. Inawezekana mtu huyu akaingia kazini ndani ya muda asubuhi, lakini anaanza kuzunguka meza moja hadi nyingine na kusimulia watu mambo yake ya nyumbani.

"Labda kuhusu sherehe ya jana au alikuwa klabu au kwenye biashara gani? Mambo ambayo hayahusiani na kazi, hizo ni dalili za kueleza huyu mtu anapitia hali gani katika afya ya akili mahali pa kazi," alisema.

Kuhusu changamoto kiakili aina ya tatu, muuguzi huyo alisema ni namna mtu alivyo na uhusiano kijamii kuanzia nyumbani, sehemu za ibada, mitaani na hata ofisini.

"Ninaposema jamii ninamaanisha ni zile sehemu zote ambazo tunaishi na jamii. Kila mtu anaishi na watu hatuishi mawinguni. Hata wafanyakazi wenzako wanaweza kukuangalia na kuhisi afya ya akili ina changamoto katika maeneo hayo matatu," alisema.

"Hii ni namna ambavyo mtu anaweza kuzikabili changamoto kijamii, kuhusiana na jamii inayomzunguka, mahala pa kazi papewe kipaumbele kuliko sehemu zingine, ingawa sehemu zote hata barabarani unapotembea, ili akili isichanganyikiwe usipate shida yoyote," aliongeza.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, mahali pa kazi ni eneo ambalo mtu hutumia muda mwingi kufanya kazi wakati mwingine saa 10 10 kati ya 24 za siku, hivyo pakitumika vizuri ni sehemu inayoweza kumtambulisha akili yake kiafya ilivyo, hasi au chanya.

"Mahali pa kazi ndiko mtu anatumia saa nyingi zaidi kuanzia nane hadi 12, ikawa ndio eneo ambalo linatumia saa nyingi zaidi. Lakini saa zilizosalia kati ya 24 matumizi yake yamegawanyika.

"Kuna kulala, kula, kuongea na familia au marafiki, mtu hutumia muda barabarani. Utakuta katika kila tukio anatumia saa mbili au nne, ila kazini ni muda halisi zaidi ya saa nane na kuendelea," alisema.

Alisema mahali pa kujitafutia riziki ambako hutumia saa nyingi, jamii inayomzunguka mhusika ni rahisi kufahamika tabia zake, kama vile kuomba mapumziko yeye binafsi, akiitaja ni dalili na ustawi duni wa akili.

"Mwingine akifika sehemu ya kazi anakutana na kazi nyingi, hivyo anaamua kulala. Haishiwi sababu nahiyo ni dalili za tatizo la akili. Mtu anajipima binafsi leo ngoja niombe ruhusa nikapumzike ni nzuri, ujue ni dalili ya akili yako inataka kutulia, kuna tatizo," alisema.

Alitoa wito kwamba mahali pa kazi ili kuepuka ustawi duni wa kiakili, kuna haja ya mtu binafsi kupima matarajio yake na kulinda afya ya akili, huku jamii ikitoa msaada kwa wanaopitia changamoto kiakili kama vile msongo wa mawazo.

"Ukiona mtu awali hakuwa hivi na umemzoa kazini alikuwa hajipambi sana, au kaanza kuvaa mavazi ambayo hayakuzoeleka yanayowaka sana rangi zake, hapo unaweza kuweka kiulizo kwa mwenzako.

"Ukiweza uanze naye taratibu ukibaini kuna tatizo kiakili tulizoea mtu anajipamba kidogo anaanza kujiremba hadi katika macho, anavaa viatu vya rangi za kuwaka, tuzungumze nao kwa upendo," alisema.

Aliongeza kuwa :"Utakuta mtu ana hisia kali labda katika michezo timu hii imefungwa hatimaye anagombana na wenziie kwa utani, au analia kirahisi, nalalamika kuumwa hapoa na pale, mtu akiingia kazini, anasema amechoka ni dalili za msongo wa mawazo ambazo ni za awali katika tatizo la akili. Au mtu anahisi harufu, sehemu hii inanuka, wengine hawahisi."

Alisisitiza jamii kufanya mazoezi baada ya kazi ili kuipa akili mawazo mapya na kuipumzisha, kula mlo wenye lishe unaozingatia mahitaji ya mwili, kwa kuwa mlo unaokwenda kinyume huchangia msongo wa mawazo.

# Masauni ataka maboresho kimfumo Jeshi la Magereza

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, amesema Jeshi la Magereza lazima likubaliane na maboresho ya kimfumo, kimuundo na kitaasisi ambayo yatakwenda kuongeza uwezo wa uzalishaji mazao ya kilimo kwa Magereza ya uzalishaji mali nchini.

Waziri Masauni aliyasema hayo juzi alipotembelea na kuzungumza na Ofisa wa Gereza la Kilimo na Mifugo Kitai, Mbinga mkoani Ruvuma.

Aidha, alisema miongoni mwa maboresho hayo ni kutenganisha mamlaka ya kiutawala ya Jeshi la Magereza na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi hilo (SHIMA).

Alisema maboresho yatakwenda kuleta ufanisi wa usimamizi wa masuala ya kiutawala na biashara.

Alitoa maagizo kwa Magereza ya uzalishaji mali nchini nzima kuchangamkia fursa za kilimo cha mazao ya nafaka kwa kutanua maeneo ya mashamba ili kuendana na jitihada za serikali katika kuinua sekta ya kilimo.

"Serikali imetanua fursa ya soko la mazao ya nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), ambayo imepewa uwezo na serikali kununua mazao kwa bei kubwa, lakini mpaka sasa bado hakuna jitihada zilizofanywa na Jeshi la Magereza kuchagamkia fursa hii," alisema.

Mhandisi Masauni alisisitiza matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuacha kitumia kuni na mkaa katika magereza, ili kuendana na ajenda ya Afrika na dunia katika kutunza mazingira.

Mkuu wa Gereza la Kilimo na Mifugo Kitai, SP. Gabriel Luderi, alisema gereza hilo lipo tayari kupokea na kuendana na mabadiliko yatakayoongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuboresha utendaji kazi.

# 200/- ilivyokatisha uhai dereva kwenye kamari

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKAZI wa Ngerengere Kaskazini wilayani Morogoro, Hussein Nyabu Steven (35), ambaye ni dereva ameuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali kifuani baada ya ubishani wa Sh. 200 na mwenzake wakati wa mchezo wa kamari.

Tukio hilo limethibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Alex Mkama, wakati akizungumza na waandishi wa habari na kubainisha kuwa mauaji hayo yalitokea juzi majira ya saa 1:00 usiku.

Kamanda Mkama alisema tukio hilo lilifanywa na Kulwa Bosco (27), maarufu kama Rasta, ambaye ni mfugaji na mkazi wa Kijiji cha Sinyaulime, Tarafa ya Ngerengere wilayani Morogoro ambaye kwa sasa anashughulikiwa na Jeshi la Polisi.

Akifafanua mauaji hayo yalivyotokea, alisema kijana huyo aliyeuawa, pamoja na mtuhumiwa walikuwa wakicheza 'pool table' na katika kubishania Sh. 200, mtuhumiwa alitoa kisu na kumchoma, hivyo kusababisha kifo.

Kamanda Mkama alitoa wito kwa wananchi hususani vijana kuacha kujichukulia sheria mkononi badala yake wafanye kazi ili kujiingizia kipato cha halali badala ya kuendeleza njia rahisi kujitafutia kipato ikiwamo kamari.



Katibu Mkuu wa Chama cha NDC, Doyo Hassan (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu mikakati ya uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja kupokea wanachama wapya. Katikati ni Mwenyekiti wa Kigoda cha Wazee Taifa wa chama hicho, Tozzy Matwanga na Makamu Mwenyekiti wa Kigoda cha Wanawake Taifa, Hadija Tambwe. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mradi kukabili upotevu mboga, nafaka wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imezindua mradi kabambe wa kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya mboga na nafaka.

Mradi huo wa miaka mitano wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 64 unaofadhiliwa na serikali ya Marekani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo (USAID), unajulikana kama Feed the Future Tanzania, Tuhifadhi Chakula.

Wakati TAHA inatekeleza mradi kwa upande wa tasnia ya horticulture, mpango wa ukuaji wa kilimo ushoroba wa kusini Tanzania (SAGCOT) unatekeleza upande wa nafaka.

Mradi unaolenga kuboresha ustawi wa wakulima, wachakataji, wafanyabiashara na wasafirishaji wa mazao ya mboga na nafaka kwa kuboresha uhifadhi wa mazao hayo na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya uhakika.

Takwimu zinaonesha kuwa hali ya upotevu wa mazao baada ya kuvuna nchini ni kati ya asilimia 30 hadi 40 kwa mazao ya mboga na asilimia 13 kwa nafaka.

Mradi wa Feed the Future Tanzania, Tuhifadhi Chakula, unakusudia kupunguza hali hiyo ya upotevu wa chakula hadi asilimia 15 kwa mazao ya mboga na asilimia saba kwa nafaka.

Akizindua mradi huo katika kijiji cha Lyamungo Kati, Hai Mkoa wa Kilimanjaro, Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema utalisaidia taifa hususan wakulima ambao wanaumizwa zaidi kutokana na upotevu wa mazao baada ya mavuno.

Silinde alisema Wizara ya Kilimo inachukua hatua mbalimbali kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo ikiwamo za tasnia za horticulture na nafaka.

Alisema baada ya kuvuna, wizara pia imeweka kipaumbele katika ujenzi wa vituo jumuishi vya kukusanya, kuchambua, kupanga madaraja, kufungisha na kisafirisha mazao ya mbogamboga katika mikoa ya Iringa, Kilimanjaro na Dar es Salaam.

"Vituo hivyo vitapunguza upotevu wa mazao ya mboga na kuendeleza ubora na mauzo ya mazao hayo ndani na nje ya nchi," alisema.

Pia alisema vipaumbele vingine vya serikali ni ujenzi wa viwanda vya usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko, na kutengeneza ajira mpya milioni 3 kwa vijana na wanawake kupitia sekta ya kilimo ifikapo mwaka 2030.

Naibu Waziri Silinde alisema serikali inatarajia mradi wa Feed the Future Tanzania, Tuhifadhi Chakula utachangia azma yake ya kuchochea maendeleo ya kilimo na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuongeza fursa za kiuchumi kwa raia wake, na kuboresha maisha ya wanufaika kwa ujumla.

Silinde aliitaka TAHA kupitia mradi wa Feed the Future kufanya kazi na serikali na wadau wengine katika kutatua changamoto zilizoko sekta ya kilimo hususan upotevu wa mazao kwa maendeleo ya tasnia ya kilimo cha mboga na matunda na nafaka.

Aidha, aliwataka wananchi wanaonufaika na mradi huo kuhakikisha wanautunza na kuusimamia kwa manufaa yao na vizazi vyao, ili waendelee kuwa na urafiki bora na wafadhili.

Awali, Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle alisema mradi wa Feed the Future Tanzania, Tuhifadhi Chakula, umekuja wakati mwafaka kwani dunia itaadhimisha siku kimataiafa ya upotevu na uharibifu wa chakula iliyotangazwa kuadhimishwa kila Septemba 29 na Baraza la Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 2020.

Alisema upotevu na uharibifu wa chakula unaziathiri familia kila nchi duniani, zikiwamo Marekani na Tanzania, ukiigharimu dunia jumla ya Dola za Marekani trilioni moja.

Balozi Battle alisema Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wanatembelea dhana ya kuwa Tanzania siyo tu kujisimamia katika usalama wa chakula, lakini pia kuwa na uwezo wa kulisha dunia inayoizunguka.

Kati ya 2018 na 2022, alisema, zaidi ya Watanzania milioni mbili walinufaika toka mpango wa chakula wa Marekani ambao uliwekekeza Dola za Kimarekani 4.8 bilioni kwenye shughuli za kilimo kuhakikisha kunakuwa na usalama wa chakula na ustawi kifedha na kiafya.

Kiongozi Mkuu wa Feed the Future, Amani Temu, alisema mradi huo utawafikia wadau takriban 931,000, akitaja baadhi ya kazi zilizokwishafanyika kuwa ni kuwajengea uwezo maofisa ugani kutokana na baadhi ya wakulima kuonekana kuwa na ufahamu zaidi yao.

Aidha, mradi umeainisha na kuibua teknolojia ambazo kuanzia mwakani zitaonyeshwa mkoa kwa mkoa ili wakulima, wachakataji na wafanyabiashara waweze kuzitumia.

Mtendaji Mkuu wa TAHA, Dk. Jacqueline Mkindi, aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuendelea kuiamini taasisi yake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi wa mitaa ni muhimu, wananchi washiriki kikamilifu

**NOVEMBA** 27, mwaka huu, Watanzania wanatarajia kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa upande wa Tanzania Bara. Uchaguzi huo hufanyika kila baada ya miaka mitano kwa ajili ya kuchagua wenyeviti wa vijiji, vitongozi na wajumbe wa serikali za vijijini huku maeneo ya mijini wakichagua wenyeviti wa mitaa na wajumbe.

Hivi sasa maandalizi ya mchakato huo yanaendelea huku viongozi mbalimbali wakiwamo wa serikali na dini wakisisitiza wananchi kujitokeza kujiandikisha na hatimaye kupiga kura. Kwa jumla msisitizo unaotolewa na viongozi hao, ni mbiu tosha kwa wananchi kushiriki uchaguzi huo ambao unashikilia hatima ya maisha yao.

Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Ruvuma, pamoja na mambo mengine, aliwahimiza wananchi kujitokeza katika kujiandikisha na hatimaye kuwapigia kura viongozi wanaofaa kuwaongoza. Msisitizo huo pia umetolewa mara kadhaa na viongozi wa ngazi za juu, akiwamo Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, akiwa katika ziara za kikazi maeneo kadhaa nchini.

Juzi pia, katika ibada maalum mjini Arusha, Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, aliwaomba viongozi wa dini kutumia madhabahu zao nyakati za ibada kuwahimiza waumini wao kujitokeza kujiandikisha ili washiriki katika uchaguzi huo. Rai hiyo iliungwa mkono na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) mstaafu, Askofu Dk. Fredrick Shoo, huku akisisitiza kuwa suala la kushiriki uchaguzi huo ni la muhimu kwa hatima ya maisha yao. Kama wahenga wasemavyo la mgambo likilia kuna jambo, mbiu inayoendelea kupigwa kuwahimiza wananchi kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa ni ya muhimu. Uchaguzi huo ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi kwa sababu viongozi wanaochaguliwa wanayajua vyema matatizo yanayowakabili wananchi, hivyo kufanyika kwake ni sehemu muhimu katika kuyatatua.

Serikali za mitaa ni chimbuko la demokrasia na utawala bora, hivyo wananchi wanapaswa kushiriki katika mchakato wa uchaguzi huo kwa kujiandikisha, kushiriki kampeni za wagombea wa vyama na kusikiliza sera zao na hatimaye kuwapigia kura. Sambamba na hayo, kiuhalisia, wananchi katika maeneo yao, kupitia viongozi wa mitaa walioawachagua, wana mamlaka ya kupanga, kuibua, na kubuni mipango yao ya maendeleo kulingana na mahitaji yao. Kwa mantiki hiyo, kushiriki katika uchaguzi kwa kuchagua viongozi wanaowataka ndiyo dira ya kupanga mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa manufaa yao.

Ni wazi kwamba wananchi katika maeneo wanayoishi, wanatambua ni matatizo gani au adha wanazokabiliana nazo. Kwa hiyo kwa kushirikiana na viongozi wao, wana uwezo wa kupanga au kutafuta namna ya kutatua matatizo hayo. Kama ni maji, elimu, barabara, afya au ukosefu wa huduma fulani, wananchi hao ndio wanaojua maumivu yanayowapata badala ya kusubiri serikali kuu ngazi ya wilaya au mkoa kuwatatulia.


Mifano hai iko katika maeneo mbalimbali ya nchi ambako wananchi kutokana na kukabiliwa na adha ya huduma husika, wameamua kuanza kuitatua na hatimaye kufika hatua fulani na kuomba msaada kutoka serikali kuu ili kumalizia na kuanza kupata huduma.

Hivi karibuni wakati wa ziara ya Naibu Waziri Mkuu Biteko mkoani Kigoma ilipobainishwa kwamba wananchi wa kata ya Kidahwe, kutokana na ukosefu wa huduma za afya, walianza ujenzi wa kituo cha afya kwa kujenga majengo na sasa wanaiomba serikali kuwasaidia umaliziaji na hatimaye kuanza kupata huduma.

Mambo hayo yanawezekana iwapo kutakuwa na msukumo wa uongozi unaowasilikiza wananchi na kushirikiana kutatua shada husika. Hali hiyo inawezekana tu kama kutakuwa na viongozi wenye utashi na watu kama hao watapatikana kwa kushiriki kuwachagua wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Kwa maana hiyo, njia pekee ya kutatua matatizo katika eneo husika ni wananchi kushiriki uchaguzi wa viongozi wenye uwezo na wenye sifa bila kujali uswahiba, undugu, urafiki, itikadi wala imani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Joyce Lameck

## Muungwana Lazima Nilonge

# Watoto hawa ni lazima wasaidiwe

**MATUKIO** ya kihalifu yanayohusisha watoto wa chini ya miaka 18, yanaibuka zaidi nyakati hizi kwa sababu wengi wao iwe mijini na vijijini wamemaliza darasa la saba.

Wengi ni wadogo na baada ya kuhitimu masomo ya msingi wanakosa cha kufanya na kujiingiza kwenye uhalifu japo wapo baadhi wanaosoma masomo ya 'pre form one' wakidokezwa watakachokwenda kufundishwa wakiingia sekondari mwakani.

Itakumbukwa kuwa yapo baadhi ya makundi ya kihalifu kama panya road yaliyokuwa yanahusisha watoto wenye umri kati ya miaka 13 na 16, ambao ni wadogo na wasioweza kuamua hatima ya maisha yao.

Lakini kuna maelezo kuwa watoto hata wakiwa wadogo wanashiriki uhalifu kama kupora mabegi na vifaa vya wenzao shuleni.

Wapo wanaotumika usiku kupenya kwenye madirisha na kuiba vitu kama simu na runinga vyumbani, hivyo wanapomaliza shule wanautumia muda huu kufanya uhalifu zaidi.

Matukio ya wadogo hao kuwa wahalifu mara nyingi yanaripotiwa katika maeneo yenye mazingira magumu kiuchumi kwenye miji na majiji kama Dar es Salaam.

Makundi ya watoto hao kwa asilimia kubwa hutoka kwenye familia na kaya maskini zisizo na uwezo wa kuwapeleka kwenye kozi mbalimbali.

Itakumbukwa mafunzo hayo ambayo yanalenga kuongeza maarifa na ujuzi wakiwa wanasubiri matokeo ya mitihani yao, yanalipiwa kuanzia Shilingi 20,000 kwa mwezi.

Kama ilivyo kawaida watoto wanaotoka kwenye familia zenye uwezo mdogo kifedha, hutumia muda huu kuwatafutia shughuli za kufanya au kuwapeleka kwenye twisheni ili kuwaongezea maarifa na ujuzi.

Pamoja na jitihada za serikali kuboresha elimu si vyema kuwaacha watoto wapotee wanapohitimu elimu ya msingi na kukosa mwelekeo kwa kushindwa kuwapatia cha kufanya kabla ya kuingia sekondari mwakani.

Juhudi za kuboresha elimu na kuitoa bure kwa watoto inafaa ilileta chachu na mwitikio mkubwa kwa wazazi na walezi kwa kuhimiza nidhamu na ufuatiliaji wa mwenendo wao katika kupenda kusoma.

Uhalifu unaojitokeza miongoni mwa wanafunzi hao wadogo waliomaliza darasa la saba kama kuvuta bangi, udokozi, ulevi, kutumia dawa za kulevya na hata kujiingiza kwenye ngono za utotoni, uiamishe jamii na serikali kufanya jambo jipya.

Ni wakati wa kutambua umuhimu wa kuandaa miradi na mafunzo mbalimbali ambayo itawasaidia watoto wenye mazingira magumu kupata mafunzo yatakayowafanya kubadilisha iwekeza nguvu na akili zao katika elimu.

Ni mbinu ya kuwafanya kuachana na makundi hatarishi wanapokuwa nyumbani kwa kipindi cha miezi mitatu, pia itasaidia kupunguza uhalifu unaohusisha vijana hawa wenye umri mdogo.

Hivyo basi ni muda sasa serikali na wadau hasa AZAKI kuandaa miradi hiyo ambayo itawasaidia watoto kupata nafasi ya kujiendeleza katika fani tofauti na kupatiwa ujuzi mbalimbali ambao utawapa fursa watakapohitaji kujiingiza kwenye mambo yasiyohusisha elimu ya nadharia.

Kama inawezekana kuwe na maelekezo kisheria ya kuwahusisha wahitimu wa kidato cha nne na cha sita kwenda kwenye mafunzo au programu mbalimbali baada ya kumaliza mitihani zikifanyika mijini na vijijini, kikiwahusisha watoto kutoka familia zenye kipato cha chini.

Ni kwa sababu watoto walio wengi wamejikuta kwenye kujifunza mambo yasiyo kuwa na tija. Mfano ni kujiingiza kwenye makundi hatarishi kama ya rika na yale ya kubeti au kucheza kamari.

Mambo hayo yanatokea kutokana na wazazi na walezi kukosa fedha za kuwapeleka kwenye kozi mbalimbali za kuwashughulisha badala ya kuwaacha kuingia kwenye uhalifu.

Ni fikra zangu kuwa kama ikiwezekana kozi za 'pre form one' zianzishwe kwenye shule zote ziwe za serikali au za binafsi lakini zisiwe na gharama kubwa, ili kila mwanafunzi aliyehitimu aweze kupata nafasi ya kusoma.

Itakuwa njia mojawapo ya kupunguza uhalifu na kudhibiti watoto wasiingie kwenye wimbi la mmomonyoko wa maadili unaoikumba dunia na taifa leo.

Wazazi na walezi kumbukeni kuwa baadhi ya wanafunzi hasa mabinti wanaweza kutumbukia kwenye mimba za utotoni na pia kudhalilishwa kijinsia.

## HABARI KITAIFA

# Wananchi Kanda ya Ziwa kufaidi huduma JKCI bure

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), imeadhimisha Siku ya Moyo Duniani kwa kuendesha kambi ya uchunguzi wa afya ya moyo bure mkoani Geita kuanzia leo.

Wiki moja kabla ya siku ya moyo duniani ambayo huadhimishwa Septemba 29, JKCI ilipeleka madaktari bingwa wanne wa moyo kwenda kufanya upasuaji kwa nchi jirani ya Zambia kama ishara ya kujenga uhusiano mzuri kati ya Zambia na Tanzania na kutoa fursa ya kujifunza na madaktari wa JKCI kufundisha wenzao wa Zambia.

Kiongozi wa ujumbe wa madaktari wa JKCI waliokuwa Zambia, Dk. Viviane Mlawi, alisema madaktari hao kwa wiki moja walitumia muda huo pia kuwajengea uwezo wa upande wa tiba ya moyo na kufungua milango Tanzania kama kituo cha umahiri wa mafunzo kwa madaktari wanaotaka kuja kujifunza Tanzania matibabu ya kibingwa ya moyo.

"Madaktari wa Zambia na wananchi wameishukuru sana Tanzania na kwa kweli wameshangazwa na umahiri wa JKCI katika tiba ya moyo kwasababu tumefanikiwa kupunguza utegemezi wa kupeleka wagonjwa wa moyo nje ya nchi kwa asilimia 95 hali hiyo imewafanya watushangae kwasababu wao hawajafika kiwango hicho," alisema.

Alisema katika mwendelezo wa kuadhimisha siku ya moyo duniani, JKCI kuanzia Oktoba 2 inapeleka wataalamu wake bingwa wa moyo mkoani Geita na wataendesha kambi ya uchunguzi wa magonjwa ya moyo bure kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa wakati wa maonesho ya madini.

Alisema hayo yote yanafanyika katika jitihada za kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ametumia gharama kubwa kuboresha afya ya mama na mtoto na huduma bora ya afya ya moyo Tanzania.

"JKCI kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Geita, imepanga kufanya uchunguzi wa magonjwa ya moyo bure na kaulimbiu ya mwaka huu inahamasisha matumizi ya teknolojia upande wa moyo kwa hiyo JKCI imeona ni wakati wa kwenda kwenye maeneo hayo ya Kanda ya Ziwa kwasababu hakuna hospitali bobezi ya moyo na ikiwezekana utafanyika utaratibu kuanzishwe kituo bobezi cha matibabu ya moyo," alisema.

Alisema, JKCI itatoa elimu ya afya ya moyo kwa wachimbaji na kuweka mkakati bora endelevu na kuhakikisha hospitali zote za Kanda ya Ziwa ikiwamo ya rufani ya Geita na Chato zinashirikiana na JKCI kuanzisha kituo kikubwa cha matibabu ya moyo.

**JKCI itatoa elimu ya afya ya moyo kwa wachimbaji na kuweka mkakati bora endelevu na kuhakikisha hospitali zote za Kanda ya Ziwa ikiwamo ya rufani ya Geita na Chato zinashirikiana na JKCI kuanzisha kituo kikubwa cha matibabu ya moyo.**



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) ambaye ni Mbunge wa Isimani, William Lukuvi, akigawa majiko kwa vijana wakati wa mashindano ya utumiaji nishati safi ya kupikia yaliyofanyika Kijiji cha Magombwe na kuhusisha vijiji vilivyoko Kata ya Mlenge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SBL, NCT waingia makubaliano fursa masomo wanafunzi 100

**Na Christina Mwakangale**

TAKRIBANI wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), watanufaika na fursa za mafunzo zilizoboreshwa katika sekta ya utalii hususan wanaosoma fani ya ukarimu.

Mafunzo hayo yamefanikiwa baada ya Serengeti Breweries Limited (SBL), kutia saini Hati ya Makubaliano (MoU) na NCT ya miaka miwili kwa lengo la kupiga hatua kuboresha mafunzo ya ujuzi wa ukarimu.

Mkurugenzi wa Mahusiano wa SBL, John Wanyancha, akizungumza kuhusu ushirikiano huo na NCT, alisema mafunzo hayo yatawawezesha vijana kufanikiwa kupitia sekta ya utalii.

"Tunafurahia kushirikiana na Chuo cha Taifa cha Utalii ili kuunda njia kwa vijana kufanikiwa katika sekta ya ukarimu."

Programu ya 'Learning for Life' (Mafunzo kwa Maisha), siyo tu kuhusu elimu, inahusu kutoa ujuzi wa maisha, utawasaidia wanafunzi kupata ajira na kuchangia ukuaji wa sekta ya utalii nchini.

Ushirikiano huu unalenga kuwapa wanafunzi na wahitimu wa ukarimu, ujuzi, muhimu na uzoefu wa vitendo ili kuchochea fursa ya ajira na kuchangia ukuaji endelevu wa sekta za utalii na ukarimu," alisema Wanyancha.

Aidha, ushirikiano huo ni sehemu ya programu hiyo, ambayo ni mpango ulio chini ya ajenda pana ya ustawi 'Spirit of Progress' iliyoundwa ili kuboresha maisha na kuunda fursa za ajira kwa vijana wa kitanzania.

Akifafanua kupitia programu hiyo, alisema wanafunzi wa NCT watapata mafunzo maalum katika ujuzi wa biashara na ukarimu, pamoja na mawasiliano, uongozi, kujitambua, upangaji bajeti na usimamizi wa muda.

"Wanafunzi watapata uzoefu wa vitendo katika shughuli za ukarimu kupitia mafunzo kwa vitendo na mafunzo ya ndani. SBL itasaidia kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa NCT katika sekta ya ukarimu, kuwapa fursa ya kujifunza kwa vitendo.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Florian Mtey, alisema ushirikiano huo ni fursa ya mabadiliko kwa wanafunzi wa NCT.

"Ushirikiano huu na SBL utaimarisha sana uzoefu wa kujifunza kwa wanafunzi wetu kwa kuchanganya maarifa ya nadharia na uzoefu wa vitendo wa sekta.

"Ujuzi na mafunzo ya vitendo watakayopata kupitia programu hii, yatawaandaa kukidhi mahitaji ya sekta ya ukarimu na utalii nchini Tanzania," alisema.

Pia, SBL itaandaa programu za mafunzo ya wakufunzi kwa wakufunzi wa NCT waliochaguliwa ili kuwasaidia kufundisha mtaala wa programu hiyo.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



## HABARI KITAIFA

# Waziri ataka e-GA kuimarisha ushirikiano zaidi sekta binafsi

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, ameitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuongeza wigo wa ajira kwa vijana wabunifu katika eneo la TEHAMA.

Sangu alitoa rai hiyo hivi karibuni, wakati akifunga programu ya awamu ya sita ya mafunzo kwa vitendo pamoja na mafunzo kazini kwa mwaka wa fedha 2024/25, inayoendeshwa na e-GA kupitia kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (e-GovRIDC), jijini Dodoma.

"Naipongeza e-GA kwa kazi nzuri mnayofanya ya kukuza vipaji na kuongeza uwezo kwa vijana katika matumizi ya TEHAMA, lakini pia ninawashauri kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kutoa fursa kwa wanafunzi wanaoshiriki mafunzo kwa vitendo pamoja na mafunzo kazini katika kituo hiki kupata fursa za ajira," alisema Sangu.

Alisema ushirikiano kati ya e-GA na sekta binafsi utaongeza tija katika kukuza na kuimarisha tasnia ya TEHAMA, na hivyo kuongeza fursa za ajira kwa vijana na hatimaye kupunguza changamoto ya ajira kwa taifa.

Hivi karibuni, baadhi ya taasisi binafsi zikiwamo benki na kampuni za simu za mkononi, zilitembelea kituo hicho na kuonesha nia ya kusaini Mkataba wa Makubaliano ya ushirikiano (MoU) katika masuala ya elimu, utafiti, na ubunifu wa TEHAMA, ikiwa ni hatua inayolenga kuimarisha ushirikiano kati ya e-GA na taasisi hizo.

"Nimetembelea miradi 'projects' mbalimbali zinazoendelea katika kituo hiki na nimeona kazi kubwa ambayo e-GA mnaifanya ya kuwaandaa vijana wetu ili waweze kuendana na mabadiliko ya teknolojia mpya zinazoibukia kama vile Akili Mnemba na Sarafu ya Kidijitali na nimeona namna vijana wetu walivyo na uwezo mkubwa katika maeneo hayo," alisema Sangu.

Aliipongeza e-GA kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha vijana wanajifunza teknolojia mpya zinazoibuka duniani.

Alisema lengo ni waweze kufanya bunifu mbalimbali za TEHAMA, ikiwa ni pamoja na kutengeneza mifumo ya kielektroniki kupitia teknolojia hizo itakayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi serikalini na utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Mafunzo haya mnayoyatoa yanawasaidia wanafunzi kuongeza ujuzi na uzoefu katika kuzielewa teknolojia mpya ili kuchochea maendeleo na mageuzi makubwa ya serikali ya kidijitali.

Aidha, alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi na kuijengea uwezo e-GA ili kuhakikisha matumizi ya TEHAMA serikalini yanazidi kuimarika sambamba na kuandaa vijana mahiri katika TEHAMA kushiriki katika ujenzi wa serikali ya kidijitali.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba, aliahidi kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi, pamoja na kuwajengea uwezo vijana katika TEHAMA ili kutoa fursa ya kuonesha uwezo wao katika TEHAMA na kushindana katika soko la ajira duniani.

"e-GA itaendeleza ushirikiano na sekta binafsi pamoja na vyuo vikuu mbalimbali ili kuwajengea uwezo vijana katika eneo la TEHAMA.



Mtaalamu wa Saikolojia, Hamis Baruani, akizungumza na wananchi wa Mtaa wa Saranga, wilayani Ubungo kuhusu namna ya kuwabaini watoto waliotendewa vitendo vya kikatili ikiwamo vya ulawiti ili kuwapa msaada haraka. **PICHA: BEATRICE MOSES**

## 'Moyo tatizo nchi uchumi wa chini'

**Na Beatrice Shayo**

ZAIDI ya wagonjwa milioni 20 wanakufa kila mwaka duniani kwasababu ya magonjwa ya moyo ambayo kwa asilimia 80 yanatokea kwenye nchi za uchumi wa kati na chini.

Hayo yalisemwa na Daktari Bingwa wa magonjwa ya moyo Tanzania na Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa wa magonjwa ya moyo, Robert Mvungi, wakati wakisherehekea siku ya moyo duniani inayosherehekewa Septemba 29, kila mwaka, iliyoandaliwa na Hospitali ya Aga Khan kwa kushirikiana na Taasisi ya Moyo Tanzania washiriki walipata punguzo la asilimia 50 kwenye chunguzi za ziada.

Dk. Mvungi alisema takribani makundi yote yanaathirika na matatizo ya moyo kutokana na uzito uliozidi kiwango cha kawaida, shinikizo la damu, kisukari, damu kuwa juu, kuvuta sigara na kutofanya mazoezi.Aidha, Dk. Mvungi alisema chama chao kitafungua kampeni ambayo itaenda mpaka vijijini na sehemu zote za nchi ili kutoa elimu kuhusu magonjwa hayo na kuchukua hatua.

Akizungumza kwa niaba ya Daktari Bingwa wa Moyo kutoka Hospitali ya Aga Khan, Dk. Julius Msukuya, alisema kati ya asilimia 25 hadi 30 ya wagonjwa ambao wanawapokea katika hospitali hiyo wana magonjwa ya moyo yakiwa ni mtambuka.

Alisema wagonjwa ambao wanawaona ni zaidi ya asilimia 30 hadi 50 wana shida ya moyo na matibabu yake yameimarika kwa kuzingatia chakula, mazoezi na usaidizi wa dawa kutoka kwa madaktari.

"Usipuuzie dalili za magonjwa ya moyo, fanya uamuzi wa haraka dhidi ya ugonjwa wa shambulizi la moyo."

# Viongozi wa vyama vya siasa watamba kushinda uchaguzi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

VIONGOZI wa vyama vya siasa Manispaa ya Morogoro, wamejigamba kuibuka na ushindi wa kishindo na wapo tayari kuzifuata na kuzingatia kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Walisema hayo baada ya kupatiwa maelekezo kuhusu uchaguzi na kanuni zake juzi kutoka kwa Msimamizi wa Uchaguzi Manispaa ya Morogoro, Emmanuel Mkongo.

Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Morogoro Mjini, Maulid Chambilila, alisema, CCM imejipanga ~~vizuri kushiriki uchaguzi wa seri-~~kali za mitaa kwa kusimamisha wagombea wake.

"Tayari tumepata taarifa kutoka kwa msimamizi wa uchaguzi wa Manispaa ya Morogoro ambaye ni mkurugenzi akiongea na sisi wadau ambao ndio wenye vyama vya siasa," alisema Chambilila.

Alisema, CCM inaamini uchaguzi ni namba, uchaguzi ni sayansi na kwamba namba zao wanaona wamezipanga vizuri na wanatarajia kwenda kushinda uchaguzi huo.

"Chama chetu cha CCM kinakwenda kushinda uchaguzi kwa matokeo ambayo kwa kazi walizozifanya za utumishi ulio bora kwa wananchi wetu," alisema Chambilila.

Katibu wa Chama cha ACT-Wazalendo Wilaya ya Morogoro, Vinnie Mtingwa, alisema chama chake kimepokea maelekezo na kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa 2024.

Mtingwa alisema ACT- Wazalendo kilijipanga tangu mapema wakitambua mwaka huu ni wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kujiandaa kiuchaguzi.

"Tunakubaliana na kanuni za uchaguzi zilizotolewa na msimamizi wa uchaguzi, kwa sababu tayari zimeshatoka," alisema Mtingwa.

Alisema ACT-Wazalendo inaingia kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kimejipanga ndani ya mitaa yote kusimamisha wagombea.

Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Wilaya ya Morogoro mjini (kichama), Elizeus Rwegasira alisema, chama hicho kilishajiandaa kuweka wagombea mitaa yote 294 na kufanya kampeni hatimaye kuibuka na ushindi.

Awali, akitoa akitoa maelekezo kuhusu uchaguzi kwa wadau, Msimamizi wa Uchaguzi Manispaa ya Morogoro, Emmanuel Mkongo, alisema, uchaguzi utafanyika kwa mujibu wa tangazo la serikali la maeneo ya utawala na mipaka yake na kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina mitaa 294.

"Maeneo haya ndiyo yatakayofanyika uchaguzi wa kuwachagua wenyeviti wa Serikali za Mitaa na wajumbe wa kamati za serikali za mitaa," alisema Mkongo.

Alisema uandikishaji wapigakura utafanyika kuanzia Oktoba 11 hadi 20, orodha ya wapigakura kubandikwa katika sehemu za matangazo ya uchaguzi Oktoba 21 na kuanzia siku hiyo hadi Oktoba 27 ni ukaguzi wa orodha ya wapigakura na Oktoba 25 ni kukoma kwa viongozi walipo madarakani.

Aidha, alisema kuanzia Oktoba 27 hadi 28 ni marekebisho ya orodha ya wapigakura, Oktoba 1 hadi 7 ni kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi, wakati Oktoba 20 hadi 26 ni mikutano ya kampeni na Novemba 27, 2024 ni siku ya uchaguzi.





# Jiji lafungua dirisha la mikopo makundi maalum

**Na Oscar Assenga,** TANGA

NEEMA ya Shilingi bilioni tatu inayotokana na makusanyo ya mapato ya ndani, imerejesha tena tabasamu la wakazi wa Jiji la Tanga, baada ya serikali kufungua dirisha la mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Jiji hilo, Juma Hamsini, wamefungua dirisha hilo kuanzia Septemba 29 mwaka huu, ambalo litakuwa wazi kwa mwezi mmoja na kufungwa Oktoba 29, mwaka huu kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi hayo maalum kupitia sera ya serikali 4-4-2.

Hamsini, alisema katika awamu hiyo, serikali imefanya maboresho ya sheria na kanuni za mikopo hiyo na kutoa wito kwa wananchi kuchangamkia fursa hiyo muhimu kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

Alisema ni muhimu wanapokuwa wamenufaika na mikopo hiyo kuchagua biashara za kufanya kwa ajili ya kuwaingizia kipato na si kuiga biashara ambazo hawana elimu nazo, hivyo kushindwa kufikia malengo yao.

"Maofisa mikopo tunakikisha tunajiepusha na undugu. Kupeana fedha hizi kwa kujuana, fuateni kanuni zilizowekwa na serikali kwa lengo la kuhakikisha walengwa wananufaika nayo," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa jiji hilo, Simon Mndende, alisema matarajio yao ni kukopesha fedha hizo kwa vikundi vya walengwa, visivyopungua 135 vilivyoko katika kata 27.

Julai mosi mwaka huu, serikali ilianza kutoa tena fedha za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri nchini baada ya kusitishwa Bungeni Dodoma Aprili 13, mwaka jana.

Katika kipindi hicho mikopo hiyo ilikuwa imesitishwa, halmashauri zilitenga fedha hizo, lakini marejesho kwa vikundi vilivyokuwa vikidaiwa yalikuwa yanaendelea.

Aprili 16, mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, alitangaza kurejeshwa kwa mikopo hiyo wakati akisoma bajeti ya wizara yake ya mwaka huu wa 2024/25.

Mchengerwa, alisema halmashauri 10 za majaribio zitaanza utoaji wa mikopo hiyo kwa kutumia benki.

**Matarajio yao ni kukopesha fedha hizo kwa vikundi vya walengwa, visivyopungua 135 vilivyoko katika kata 27.**

# Serikali yasikia kilio wakulima, wafanyabiashara wa dengu

**Na Jaliwason Jasson,**

HANANG'

SAKATA la wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya dengu na mbaazi wilayani hapa Mkoa wa Manyara kuandamana kushinikiza serikali kutoa tamko kuhusu ucheleweshwaji wa malipo kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, limechukua sura mpya.

Ni baada ya Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Almish Hazali, kulieleza Nipashe kuwa serikali imeanza kushughulikia haraka changamoto hiyo na kuwataka wakulima na wafanyabiashara kuwa na subira.

**Kitendo cha serikali kuwawekea masharti ya kuuza na kusubiri malipo kwa mfumo huo ni jambo gumu kwao.**

Mwishoni mwa wiki iliyopita, wakulima na wafanyabiashara hao, waliandamana na kufunga barabara kuu ya Babati/ Singida katika eneo la Masakta kwa zaidi ya saa mbili na kusababisha kusimama kwa muda shughuli za usafirishaji.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Makarani Ahmed, jeshi hilo lilifanikiwa kuwaondoa wakulima, wafanyabiashara na kuondoa vizuizi vilivyokuwa barabarani ili kupisha shughuli za usafirishaji kuendelea.

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima, akiwamo Paul Mayo, alisema wamechukua hatua hiyo ili kuishindikiza serikali kuwapa uhuru wa kuuza mazao yao na kujiingizia kipato.

Mayo, alisema kuwabana kwa kuwapangia wauze kwa mfumo huo ni kukwamisha maendeleo yao kwa kuwa wengi wao wanajiandaa kuanza msimu mpya wa kilimo.

Violet Samweli, alisema kitendo cha serikali kuwawekea masharti ya kuuza na kusubiri malipo kwa mfumo huo ni jambo gumu kwao na kuitaka iwaache wawe na soko huru ili kuruhusu mazao yauzwe na halmashauri kukusanya ushuru kwa wanunuzi.

Violet, alisema wanategemea dengu na mbaazi kama mazao ya biashara, hivyo wakiwekewa masharti magumu, kilimo kwao kitakuwa hakina faida.



Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, akisalimiana na viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, jana wakati akiwasili katika uwanja wa Jitegemee kuzungumza na walimu, viongozi na wananchi katika sherehe za uzinduzi wa Kampeni ya Mtoto wa Leo Samia wa Kesho. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TARURA yaagizwa kukarabati barabara

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ameiagiza Ofisi ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kufanya ukarabati wa dharura wa barabara ya Rafael hadi Umbwe Sekondari.

Eneo hilo lina huduma za jamii, ikiwamo hospitali na Shule ya Sekondari ya Umbwe.

Babu alitoa agizo hilo juzi, baada ya kuzindua maadhimisho ya Jubilei ya miaka 75 ya Umbwe Sekondari wakati akijibu malalamiko ya wananchi kuhusu ubovu wa barabara hiyo.

"Nimepita hiyo barabara nimejionea taasisi mbalimbali zinazowasaidia jamii, ikiwamo shule na hospitali. Naagiza TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kufika na kufanya ukarabati haraka iwezekanavyo," alisema Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Raymond Mwagala kwa niaba ya Babu na kusisitiza kuwa:

"TARURA mfike na kuona ni kwa namna gani mnavyoweza kutumia fedha za dharura kuirejesha katika hali ya kawaida barabara hii ili isiendelee kuathiri shughuli za kiuchumi na utaoji wa huduma za jamii."

Vilevile, aliagiza Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kuhakikisha Umbwe inapata vitabu kulingana na mahitaji ili iweze kufanya vizuri zaidi katika ufaulu wa mitihani ya kitaifa.

Jubilei hiyo ya miaka 75 ya Umbwe, inatanguliwa na kauli mbiu isemayo, 'mti safi, huzaa matunda bora'. Kilele chake ni Novemba 9, mwaka huu, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mkuu wa Shule hiyo, Elirehema Mungaya, akitoa taarifa kuhusu maandalizi ya kumbukizi hiyo kwa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Raymond Mangwala, alisema sekondari hiyo iliyoanzishwa mwaka 1949 hadi sasa ina wanafunzi 688 wa kidato cha tano na sita.

"Mheshimiwa Kaimu Mkuu wa Mkoa, tumekuwa tukipokea fedha serikalini kutoka mwaka 2019 hadi 2023 ambayo ni zaidi ya bilioni 1.3 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu," alisema Mungaya.



# Madiwani wakwamisha kilimo cha pamba Simiyu

**Na Alex Sayi,** MASWA

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Kenani Kihongosi, amewaonya baadhi ya madiwani kwa madai ya kukwamisha kilimo cha pamba kwa kuingilia utoaji wa pembejeo kwa wakulima kwa manufaa binafsi.

Kihongosi alitoa onyo hilo wakati wa ziara yake ya kikazi wilayani hapa baada ya kupokea taarifa za madiwani kuingilia mchakato huo na kusababisha kilimo hicho kuzidi kudorola.

Alisema madiwani hao wamekuwa na tabia ya kuingilia ugawaji wa pembejeo na viwatilifu kwa kupenyeza majina ya wasiokuwa wakulima na kusababisha walengwa kutokufikiwa na mpango huo.

"Wanafanya ubadhirifu huu kwa wakulima wakielekeza pembejeo hizo kwa watu ambao sio wakulima wa zao hilo... nawaomba acheni kuingilia zoezi hili," alionya Kihongosi.

Diwani wa Ngulinguli, Peter Mlyandingu, aliliambia Nipashe kuwa malalamiko hayo yana ukweli kutokana na madiwani hao kutumia nguvu ya kisiasa kuingilia na kusababisha walengwa kukosa pembejeo hizo.

Akizungumza na Nipashe kwa sharti la kutotaja jina, mmoja wa maofisa kilimo kata, alisema madiwani hao wamekuwa wakitumia ubabe na nguvu za kisiasa kuingilia mchakato huo.

"Katani kwangu mpaka sasa sielewani na diwani maana nilimkatalia kuingilia majukumu yangu, hivyo alinishtaki kwa mkurugenzi nifukuzwe kazi, akashindwa na siku moja nilihojiwa na watu wa usalama nikituhumiwa kuwa mwanachama wa upinzani," alidai ofisa huyo.

## Serikali yapigia debe mikopo ya vikundi TASAF

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imezielekeza halmashauri mkoani Tabora kutoa kipaumbele cha kupata mikopo kwa vikundi vya akiba na mikopo vinavyoundwa na walengwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea miradi ya TASAF mwishoni mwa wiki iliyopita mkoani humo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Nchi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, alisema vikundi hivyo vinastahili kupewa mikopo kwa kuwa wamepewa elimu ya ujasiriamali kupitia TASAF na vimehakikishwa kuwa na nidhamu katika ukopaji na ulipaji.

"TASAF inasaidia walengwa wake kuanzisha na kuendesha vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana na kufanya shughuli za ujasiriamali ii kukuza uchumi wa kaya zao, halmashauri za Mkoa wa Tabora ziangalie namna ya kufanikisha walengwa hawa kupata mikopo wanayoitoa ili kuongeza tija kwenye shughuli zao za kukuza uchumi wa kaya zao," alisema Sangu.

Akizungumzia mpango wa ajira za muda kwa walengwa, alisema utasaidia kupunguza umaskini na ni fursa kwa walengwa kujifunza ujasiriamali na ufundi kwa ajili ya kuwasaidia katika maisha yao ya kila siku.

Alikumbushia utaratibu na sheria za ajira za muda na kusema kuwa wazee kuanzia miaka 65 na kuendelea, watoto chini ya miaka 18, wajawazito na watu wenye ulemavu hawaruhusiwi kujihusisha na kazi hizo.

"Kaya za walengwa ambazo zina vijana waliomaliza kidato cha sita na wana vigezo vya kujiunga na masomo ya elimu ya juu, watoe taarifa TASAF ili wapewe barua kuambatanisha na maombi ya mkopo wa asilimia 100 ili uwasaidie kwenye masomo yao," alisema.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu (katikati), akizungumza na wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mkoani Tabora, alipotembelea kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa na mfuko huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kaya 9,000 zaaga umaskini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KAYA 9,245 mkoani hapa zimeondolewa katika mpango wa kunusuru kaya maskini wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) baada ya kuimarika kiuchumi.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa TASAF mkoani hapa, Dotto Maligisa, wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mpango huo wa mfuko huo awamu ya pili.

Maligisa, alisema wakati mpango huo unaanzishwa mkoani hapa mwaka 2015 walikuwa na kaya 44,370, lakini kwa sasa 9,245 zimeimarika kiuchumi kupitia ruzuku za fedha ambazo walikuwa wakipewa, hivyo kuondolewa na kusalia 35,325.

"Katika mpango wa TASAF awamu ijayo zitaingizwa kaya zingine," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, alisema katika mkoa huo, Sh. bilioni 60 zimetolewa kwa walengwa wa TASAF ili kuimarisha uchumi wa kaya zao.

Macha, aliwasihi walengwa ambao bado wapo kwenye mpango huo, kutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ili waondokane na umaskini.

Mkurugenzi wa Uratibu wa TASAF, Haika Shayo, alisema mpango wa TASAF awamu ya pili, ulianza mwaka 2021 na unatarajia kufikia kikomo Septemba mwakani.

Haika, alisema wamefanya tathmini na kubaini nchi nzima walengwa 300,000 wamehitimu kwenye mpango huo baada ya kaya zao kuimarika kiuchumi.

Aliwataka wanufaika ambao wamehitimu kwenye mpango huo kuendelea kuwa kwenye vikundi vya akiba na kuwekeza ili kujiimarisha zaidi kiuchumi.

## Sangoma 'stop' kutibu kichaa cha mbwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAGANGA wa jadi maarufu sangoma wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga wamepigwa marufuku kutoa matibabu kwa watu wanaong'atwa na mbwa mwenye kichaa ili kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huo katika jamii.

Amri hiyo imetolewa baada ya kuwepo kwa taarifa kuwa waganga hao wamekuwa wakihusisha suala hilo na imani za kishirikina na kusababisha watu kufa kwa ugonjwa huo kutokana na kuchelewa kwenda hospitalini kupata tiba.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, Dk. Damian Kilyanyi, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Magereza.

Dk. Kilyanyi, alisema kitendo cha waganga hao kupokea wagonjwa hao, kimekuwa kikisababisha ongezeko la vifo vya watu wanaong'atwa na mbwa.

Alisema waganga hao wamekuwa chanzo cha watu wanaong'atwa mbwa kufa baada ya kuchelewa kupata matibabu hospitalini kutokana na imani za kishirikiana hasa kwa wanaoishi vijijini.

Alisema kwa mwaka jana katika Kata ya Kilago kuna mtu aling'atwa na mbwa badala ya kwenda hospitali kupata tiba, alipelekwa kwa mganga wa jadi.

Alisema mganga huyo alimweleza kuwa aliyemng'ata sio mbwa na baada ya kuona hali imeanza kuwa mbaya, alimkimbia mgonjwa huyo.

"Mwaka huo pia mwanafunzi wa darasa la nne mkazi wa Lugela alipoteza maisha baada ya kung'atwa na mbwa kwa kuchelewa kupata tiba, kila alipokuwa akiwaeleza wazazi wake walikuwa hawachukulii suala lake kwa uzito mpaka pale alipofikia hatua ya kuanza kubweka kama mbwa. Kila mmoja ana wajibu wa kuchukua hatua za haraka," alisema.

Alisema kichaa cha mbwa hakitibiwi kwa mganga wa jadi, mtu anapong'atwa na mbwa, anatakiwa kuwahimishwa hospitali au kituo cha afya kupata tiba kisha kutoa taarifa ofisi za mifugo ili kumdhibiti mbwa huyo asiendelee kuleta madhara kwa watu wengine.

Mtaalamu wa wanyama kutoka TAPO, Abdulmariki George, alisema kila mwaka wamekuwa wakitoa chanjo ya mbwa na paka bure ili kupambana na ugonjwa huo unaosababisha watu kufa kwa kuchelewa kupata matibabu hospitalini.

Mratibu wa Shirikisho la Tiba Asili Kanda ya Magharibi, Athumani Waziri, alisema ni kosa waganga hao na wa tiba mbadala kuwapokea wagonjwa kuwapatia matibabu ambayo wana uhakika hawawezi kupona.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 1, 2024
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




Ukurasa 12

**Hawa ndiyo viumbe hatari zaidi kwa mwanadamu kote duniani**




Ukurasa 13

CBE ilivyotumia ubia PPP kuboresha elimu



Ukurasa 14

**PEMBA YA KIJANI**
Ulinzi wa misitu kwa kufuata mila na desturi za jamii, jadi

ELIMU
**NA SABATO KASIKA**

## RED CROSS LIPO TATIZO BARABARANI

# Madereva hawana elimu kutoa huduma ya kwanza, kuwafunza sheria za usalama, kuhudumia majeruhi

UKOSEFU wa elimu ya usalama barabarani kwa baadhi ya watumiaji wa vyombo vya moto, ni moja ya visababishi vya ajali zinazoendelea kuripotiwa kila wakati.

Ni kwa mujibu wa Kitengo cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi kinachofafanua zaidi kuwa pamoja na ukosefu wa elimu hiyo, kupuuza na kutokufuata sheria za usalama barabarani nalo ni tatizo.

Mkuu wa Mafunzo Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Dinaah Mosy, anasema jeshi hilo mara kwa mara linatoa elimu kuhusu utii wa sheria za usalama barabarani.

Anafafanua kuwa pamoja na juhudi hizo wapo baadhi ya madereva wa bodaboda ambao hawana nidhamu wala hawazingatii sheria ambazo pia zinawaelekeza kwenda kusomea udereva.

"Licha ya jeshi kuwaelimisha, baadhi yao hawazingatii, wapo wanaojifunza udereva usiku vichochoroni, kisha asubuhi wanaingia barabarani kubeba abiria," anasema Dinnah.




Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Dinnah Mosy, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mafunzo hayo. **PICHA: SABATO KASIKA**

Dinnah anasema hatua hiyo inahatarisha maisha yao na ya abiria kila wanapotoa huduma na kuongeza wingi wa ajali ambazo kuanzia Juni mwaka 2023 hadi Julai mwaka huu zimefikia 163,148, huku asilimia 61 ya majeruhi wakiwa ni wa bodaboda.

Anasema hayo ni kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dk. John Jingu , wakati akizungumza katika semina na wadau wa usafirishaji inayofanyika jijini Dodoma hivi karibuni.

Lakini Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Madereva wa Bodaboda na Bajaj mkoa wa Dar es Salaam na Taifa, Said Kagoma, anasema tatizo la kukimbia mafunzo linatokana na gharama kubwa wanachama wake wanazotozwa ili kujifunza taalamu hiyo.

Anasema kwa Dar es Salaam kuna madereva zaidi ya 200,000, wakati kitaifa kuna madereva zaidi 2,000,000 na kufanana kuwa chanzo cha madereva wengi kujifunzia udereva uchochoroni ni ada kubwa inayoanzia Sh. 180,000 kwa mwezi wanayolipa vyuoni.

"Kama vyuo vya udereva kama VETA Chang'ombe na Buza vyote vya Dar es Salaam, Vikindu na Kibaha mkoani Pwani, ambavyo tunasoma kwa miezi mitatu kabla ya kuingia barabarani, gharama zake ni hizo ambazo hatuwezi kumudu tutasemaje sisi wanyonge," anasema.

Anafafanua kuwa, kwa siku dereva anaweza kupata Shilingi 25,000 hadi 30,000 na kupeleka kwa bosi Shilingi 10,000 au 12,000 kisha anatoa pesa ya mafuta 7,000 na kubakiwa na kiasi kidogo.

"Kinachobaki hakiwezi kutosha matumizi ya nyumbani na kulipia ada ya kujifunza udereva, ndio maana tunaomba tupunguziwe, ili wengi wasome na waweze kufanya kazi yao kwa weledi," anasema.

Kagoma anasema, wao hawawezi kujilinganisha na madereva wa Bolt au Farasi, kwa maelezo kuwa wenzao hao wanafanya kazi kwa mtandao, tofauti na wao (bodaboda), wanaoshinda sehemu moja wakisubiri abiria.

"Kwanza wenzetu hao hawakamatwi kama sisi, lakini pia wanazunguka jiji zima bila usumbufu, kwani wanaweza kufikisha abiria sehemu fulani wakaitwa sehemu. Hivyo nzima wanakuwa na abiria ingawa sijui wanaingiza kiasi gani cha fedha kwa kutwa," anasema.

**RED CROSS KAZINI**

Kutokana na upungufu na hatari hiyo inayojitokeza, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (Red Cross), kinakusudia kuwaelimisha madereva wa bodaboda wa Dar es Salaam katika jitihada za kupunguza ajali hizo.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Matawi ya Red Cross Tanzania, Reginald Muhango , anasema na kuongeza kuwa chama kitaanza kutoa elimu itakayoambatana na mafunzo ya huduma ya kwanza.

Anasema ni jukumu linaloanza mwezi huu hadi Desemba, wakishirikiana na wadau mbalimbali, wakiwamo polisi na kiwanda cha bia cha TBL wanaofadhili mradi huo.

Muhongo anaeleza hayo wakati wa uzinduzi wa mpango wa kutoa mafunzo kwa madereva hao wiki iliyopita. Kwamba watajikita zaidi kwenye mafunzo ya kutoa huduma ya kwanza huku kikosi cha usalama barabarani wakifundisha udereva na sheria ya usalama barabarani.

Anaeleza kuwa pamoja na madereva wengi kutozingatia sheria za usalama barabarani, wamegundua kuwa kuna tatizo kwenye kusaidia wanaojeruhiwa kwenye huduma ya kwanza inapotokea ajali na sasa wanakwenda kulifanyia kazi kupitia elimu watakayotoa.

"Tunakwenda kuwaelimisha ili wanapopata ajali au wakikuta mtu amepata ajali wajue jinsi ya kumhudumia kabla ya kumfikisha hospitalini. Wengi wakifika eneo la ajali hushangaa badala ya kutoa

INAENDELEA UK. 13

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Hawa ndiyo viumbe hatari zaidi kwa mwanadamu kote duniani

WENGI wanaweza kuwaza kuwa ni simba na mamba, au chui ama tembo lakini, wanyama wengi hawana hatari kuliko inavyotarajia. Mfano papa, huua wanadamu 70 kila mwaka.

Inashangaza kwamba viumbe hatari zaidi duniani mara nyingi ni vidogo zaidi lakini vina uwezekano mkubwa wa kuua kwa magonjwa na sumu badala ya meno yenye ncha kali.

Mfano virusi kama vya homa ya ini, ebola na Corona ni vitu vinavyotisha ila havina meno wala ukubwa wa mwili.

Kiumbe hatari au namba moja kwa mauaji ni mbu huua watu takribani 725,000 kwa mwaka. Ndiye mdudu hatari zaidi duniani huangamiza wazee kwa vijana kupitia magonjwa yanayoeneza kama vile malaria. Mbu jike pekee anauma na kuleta hatari zaidi.

Kupitia uwezo wao wa juu wa kuua, mdudu huyu mdogo anayeruka ameongoza kuua wanadamu na kwa miaka mingi. Maambukizi ya malaria ni hatari Afrika, huku eneo hilo likiwa na asilimia 95 ya wagonjwa na asilimia 96 ya vifo kote duniani.



Viboko licha ya ukubwa hawana athari mbaya kwa binadamu kama alivyo mbu. **PICHA: BBC.**

### BINADAMU WAMO

Wanadamu husababisha vifo 400,000 kwa mwaka. Ni wanyama wa pili hatari zaidi duniani linapokuja suala la vifo vya watu. Japo ndiye anayehesabu mauaji. Ndiye anayeua zaidi pia.

Asilimia 0.7 ya vifo mwaka 2019 vilitokana na mauaji. Amerika ya Kusini, viwango vya mauaji ni vya juu zaidi kuliko sehemu nyingine zozote duniani na mauaji yanachangia zaidi ya asilimia saba ya vifo nchini El Salvador.

Wanadamu hawako peke yao katika kuuana wenyewe.

Ni bora kuepuka mbu iwezekanavyo kwa kununua na kufunga chandarua ikiwa unapanga kusafiri katika maeneo ambayo wadudu ni tatizo, unaweza kujikinga pia lakini si kwa binadamu.

Nyoka wamo huua watu 138,000 kwa mwaka, lakini ni nyoka wa aina gani?

Nyoka hatari wanaweza kupatikana duniani kote na wanaweza kuua wanadamu kwa njia tofauti na za kikatili. Mfano koboko (black mamba), anaweza kuua binadamu kwa matone mawili ya sumu ilhali chatu wanaweza kummeza mtu mzima.

Chatu hushambulia kwa kuzungusha miili yao mirefu kuzunguka na kubana mawindo yao, na kuwakosesha pumzi na kuvunja mifupa hasa mbavu.

Kisha hutumia taya zilizonyooshwa kumeza. Ndiyo, wanakua wakubwa vya kutosha kumeza mtu mzima, na chatu wanaojulikana hukua hadi mita 10 kwa urefu.

Wengi wanamfahamu kunguni kwa harufu mbaya lakini ni hatari anasababisha ugonjwa wa chagas, unaoua watu 100,000 kwa mwaka.

Pia wapo mbwa wenye kichaa wakiwaua watu 59,000 kwa mwaka. Japo ni rafiki bora wa mwanadamu anaweza kuwa adui mbaya zaidi wa mtu linapokuja suala la kichaa cha mbwa.

Mbwa wanapenda kuwalinda wamiliki wao dhidi ya wavamizi na watashambulia kwa kuuma. Wakati vifo vinavyotokana na kushambuliwa na mbwa si vya kawaida, mauaji ya binadamu kutokana na kichaa cha mbwa kinachoenezwa kwa kuumwa na mbwa si jambo la kawaida kusikika.

Vifo vinatokea katika sehemu wanapoishi maskini zaidi za dunia ikiwa ni pamoja na Afrika na Asia.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema :"Mbwa ndio chanzo kikuu cha vifo vitokanavyo na kichaa na hivyo kuchangia hadi asilimia 99 ya maambukizi yote ya kichaa cha mbwa kwa wanadamu."

Kichaa huambukizwa kwa mate kupitia kuumwa, mikwaruzo na kugusa moja kwa moja na maeneo yaliyoambukizwa kwenye mbwa.

Ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni, nge naye yupo anayewaua watu 3,300 kwa mwaka.

Wadudu hawa wa kale watambao na wakali huuma na mkia wao na kuingiza sumu kwenye mawindo yao. Pamoja na kuwapo zaidi ya spishi 2,600, karibu 25 pekee hubeba sumu yenye nguvu ya kutosha kuua wanadamu.

Sumu huua vijana, wazee na wale walio na matatizo ya kiafya yanayoendelea ikiwa ni pamoja na magonjwa ya moyo. Binadamu wazima wenye afya njema wanaweza kuuawa kwa kuumwa pia hasa nchi za Amerika ya Kusini.



Mamba nao wamo huua watu 1,000. Ni mnyama mkali ambaye husababisha hadi vifo 1,000 vinavyoripotiwa kwa mwaka. Kumuangalia meno kunapaswa kukuambia kwa nini wanyama hawa watambaao ni hatari.

Mfano mamba wa Mto Nile ana nguvu ya kuuma zaidi ana nguvu zaidi kuliko mnyama yeyote duniani, huku mamba wa maji ya chumvi akiwa na nguvu kidogo.

Mamba ni wakali na hushambulia kitu chochote kinachoingia kwenye makazi yao, mara nyingi huvizia mawindo wakiwa majini.

Tembo wamo, huua watu 600 kwa mwaka.

Anaangamiza idadi hiyo licha licha ya kwamba ni mnyama hatari zaidi na hodari duniani kutokana na ukubwa wake.

Anaweza kuwashambulia wanadamu kwa njia mbalimbali. Kwa kawaida huwaua kwa kuwakanyaga. Kwa vile tembo wa Afrika anaweza kuwa na uzito wa tani nnne lakini wale wa Asia hadi tani tano na nusu.

Tembo pia anaweza kutumia mkonga wake kuwaburuza na kuwatupa wanadamu mbali kisha kuwavunjavunja akiwakanyaga chini ardhini. Inawezekana pia, kwa tembo kupiga watu kwa kutumia meno na kuwaumiza hata kuua.

Viboko huua watu 500 kwa mwaka. Wapo kwenye orodha hii kutokana na kuwa wala nyasi, lakini kiasili ni mojawapo ya wanyama hatari zaidi duniani.

Viboko hutumia meno yenye ncha kali karibu nusu mita kupigana na kuuma kiumbe, kukata mwili wa mwanadamu katikati. Anauma kwa nguvu karibu mara tatu ya simba.

Wakiwa katika eneo lao, viboko wanaweza kushambulia binadamu anapokaribia makazi yake na wanajulikana kushambulia boti ili kujilinda wakifananisha na wanyama wanaowinda. Kiboko anajulikana kula wanyama wa aina yake kutokana na kukata tamaa.

Simba naye yupo anatajwa kuwa ni mwamba wa porini, ambaye anaishi mbugani ni mwindaji mkali

hushambulia wakati wa usiku kwa kutumia makucha makali na kusababisha majeraha makubwa na kwa kuuma na kung'ata mifupa na fuvu la kichwa.

***BBC***

ELIMU

NA DK. REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# CBE ilivyotumia ubia PPP kuboresha elimu

MAENDELEO ni lazima, lakini yasipogusa maisha ya watu hayana maana, ni sharti yawaguse wananchi na kubadilisha maisha yao.

Kuboresha maisha ya watu ni pamoja na kuwapa elimu bora, huduma bora za afya, maji, umeme, barabara, masoko, ajira, uwekezaji na uhakika wa chakula ili kumgusa kila mmoja na asiachwe hata mmoja.

Kimsingi, serikali inawajibika moja kwa moja kwa wananchi kwa kuwapatia maendeleo kupitia kupanga na kutekeleza miradi kwa mujibu wa dira, vipaumbele, miradi ya kimkakati na kwa maelekezo ya katiba ili kufikia ustawi wa maisha ya raia.

Miongoni mwa jambo ambalo limepewa msukumo mkubwa na serikali ya awamu ya sita ni ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi - PPP. Kuanzia 2022, Rais Samia Suluhu Hassna, anamteua David Kafulila kuwa kamishna wa PPP ili kuwe na msukumo wa kipekee katika ushirikiano wa maeneo hayo kwa lengo la kufikia ustawi wa wananchi.

Ni ukweli kuwa ujenzi wa taifa unahitaji juhudi za pamoja. Wakati mwingine baadhi ya wananchi wamekuwa na dhana potofu kuwa serikali peke ndiyo yenye wajibu wa kufanya kila kitu bila kujua kuwa hata mtu binafsi, kampuni na AZAKI ni sehemu ya ujenzi wa nchi.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa miradi ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi inaibuliwa ili kutatua kero za wananchi badala ya kutegemea na kusubiria fedha kutoka serikalini pekee kuboresha maisha ya Watanzania.

Sekta binafsi ni mdau muhimu wa maendeleo na pale inapokuwa imara mchango wake unakuwa mkubwa na hivyo maisha ya wananchi wanakuwa bora zaidi. Ndiyo maana zama hizi kunahitajika uzoefu, utaalamu na raslimali fedha za kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo.




Chuo cha CBE kampasi ya Dar es Salaam, kinavyoelekea kumaliza tatizo la uhaba wa mabweni. **PICHA: MTANDAO**

Hivi karibuni Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Dodoma kwa kushirikiana na Kituo cha Ubia wa Sekta za Umma na Binafsi (PPP) wameshirikiana ili kufanikisha azma ya kujenga mabweni ya wanafunzi kwa ubia yakigharimu Shilingi bilioni 20.7.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Chuo cha CBE, Prof. Edda Lwoga, ubia huo unatokana na changamoto ya mabweni katika kampasi kuu ya jijini Dar es Salaam na kwamba chuo kina wanafunzi 12,000 lakini mabweni yaliyopo ni mawili yenye uwezo wa kuchukua vitanda 160 pekee vya wanafunzi wa kike na kiume.

Vitanda hivi 160 ni sawa na asilimia 1.34 huku kukiwa na upungufu wa vitanda kwa asilimia 98.6, anaongea Profesa Lwoga.

"Mradi huo utafanywa kwa ubia kati ya CBE na mwekezaji lakini pia naomba nitumie nafasi kuwafahamisha wadau, wawekezaji wa ndani na nje kuhusu fursa hii muhimu ya uwekezaji ili waweze kushiriki kwenye mkutano maalumu utakaokutanisha wadau mbalimbali katika kuupelekea mradi huu sokoni na kupeana uelewa zaidi...," anasema Profesa Edda.

Ubia kati ya serikali na sekta binafsi ni muhimu kutokana na uwepo wa changamoto katika sekta ya elimu kama vile upungufu wa madarasa, madawati, meza, viti na samani nyingine, mabweni, mabwalo, nyumba za walimu, kumbi za shule, mafunzo kazini kwa walimu na vifaa vya TEHAMA. Nguvu ya pamoja baina ya sekta hizi mbili inachagiza utatuzi wa changamoto katika sekta ya elimu.

Uhitaji mkubwa wa mabweni katika chuo cha CBE utapungua kutoka asilimia 1.34 iliyopo sasa hadi asilimia 30 mradi huo wa ujenzi wa mabweni utakapokamilika.

"Hali iliyopo imesababisha uhitaji mkubwa wa malazi ya wanafunzi kwa asilimia 98.6 hivyo wengi wanalazimika kutafuta malazi nje ya chuo kwa gharama kubwa, jambo linalosababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kumudu. Njia ya PPP ni bora na ya haraka kufanikisha mradi huu, ambayo itawanufaisha wanafunzi.

CBE imejikita katika kutoa mazingira bora ya kujifunzia na kuboresha malazi ya wanafunzi ni kipaumbele muhimu kwetu nawashukuru washirika wa sekta binafsi, serikali na wadau wote kwa mchango wao katika kufanikisha mradi huu muhimu, anasema Prof. Edda.

Mwezi uliopita Kamishna wa PPP, Dk. Kafulika, anausifu ubunifu uliofanywa na CBE katika kutatua changamoto ya mabweni, na hivyo kutoa wito kwa vyuo vingine kuihusisha sekta binafsi katika ujenzi wa mabweni na miradi mingine ya maendeleo.

"Kila mradi ambao sekta binafsi inaweza kuutekeleza kwa teknolojia ya hali ya juu kuliko serikali basi ipewe nafasi ili tujenge uchumi wa kisasa ambao sekta binafsi ndiyo ina nafasi kubwa ya kutengeneza ajira nyingi. Utaratibu wa ubia unaleta unafuu kwa serikali kwa sababu miradi inajengwa bila kutegemea fedha zake lakini utaratibu huu wa ubia unafanya serikali ivute teknolojia ya kujenga baadhi ya miradi, teknolojia ambayo kwa kiasi kikubwa inapatikana sekta binafsi," anasema Kafulila.

Sekta binafsi ina nguvu ya fedha, ujuzi, uzoefu na teknolojia katika kumudu majukumu ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya elimu. Kwahiyo, ni muhimu kwa viongozi serikalini kuishirikisha ipasavyo katika miradi mbalimbali ya elimu ili kuboresha sekta ya elimu.

Sanjari na hilo, ni muhimu kuzingatia kuwa ubia kati ya serikali na sekta binafsi si ubinafsishaji, unaolenga kuunganisha nguvu ya pamoja, miradi ya ubia inabaki kuwa mali ya serikali, huku sekta binafsi ikiwa mshirika muhimu, na baada ya kurejesha gharama zake za uwekezaji kwa mujibu wa mikataba, serikali ni mmiliki kwa asilimia 100.

Ni vyema sekta binafsi ikapewa ushirikiano badala ya kuwekewa vigingi katika kuboresha elimu kwani ni wadau muhimu kwa maendeleo. Naamini miradi ya ubia katika eneo hilo ni muhimu kuanzia elimu ya awali, sekondari, vyuo vya kati hadi juu.

**Mwandishi ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali mkoani Dodoma.**
**Maoni: 0620 800 462**

## MADEREVA HAWANA ELIMU KUTOA HUDUMA YA KWANZA, KUWAFUNZA SHERIA ZA USALAMA, KUHUDUMIA MAJERUHI

**INATOKA UK.11**

huduma kwa majeruhi," anasema Muhango.

**RED CROSS WANACHOLENGA**

Anasema, elimu hiyo itaanza kutolewa wakati wowote kuanzia mwezi huu kwa kushirikisha madereva wa bodaboda, viongozi wa serikali za mitaa, kata tarafa, wilaya hadi mkoa, kupitia mikutano.

"Tutafika wilaya zote tano za Dar es Salaam na kuitisha mikutano kwa ajili ya kutoa elimu kwa madereva na viongozi wao na wa serikali wakishiriki, kwani nao wanatakiwa kupata elimu hii," anasema Muhango.

Mkufunzi wa Huduma ya Kwanza wa Msalaba Mwekundu, Peter Bongo, anasema, chama hicho kimegundua kuwa madereva wa boda na abiria wao hawafahamu jinsi ya kutoa huduma ya kwanza wakati wa ajali. Anasema kabla ya kutoa huduma cha kwanza ni kujali usalama wa wote mtoa huduma na majeruhi na wengine walio katika tukio na kwamba mara nyingi unapotokea ajali, watu hukusanyika bila tahadhari.

Bongo anasema hakikishi mazingira yako salama, huku akiongeza kuwa katika mazingira hayo, inaweza kutokea ajali nyingine, hivyo, mtoa huduma anatakiwa kuwaelekeza watu wawe makini wasije kuumia tena.

"Baada ya kujihakikishia usalama, ataomba msaada wa usafiri kisha mtoa huduma ya kwanza atamfanyia tathmini majeruhi kujua ana tatizo gani kwani ni muhimu kutoa huduma baada ya kujua ukubwa wa tatizo ili iwe rahisi kumhudumia," anasema Bongo. Mkufunzi huyo anasema kinachofuata ni kuanza kutoa huduma ya kwanza na kwamba ni lazima ifanyike haraka kuokoa maisha ya majeruhi.

"Madereva wengi hawana elimu mfano kumbeba majeruhi asiumie zaidi. Hivyo, Red Cross tunakwenda kuwaelimisha, wajue jinsi ya kutoa huduma ya kwanza," anasema.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

PEMBA YA KIJANI

# Ulinzi wa misitu kwa kufuata mila na desturi za jamii, jadi



Misitu ya mikoko inayopunguza makali ya athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kukata kasi ya mawimbi ni rasilimali muhimu Pemba. **PICHA: MTANDAO**

KUTUMIA mila na desturi kulinda misitu na hifadhi za maji ni jambo linalowezekana, ushuhuda ukitokea kisiwani Pemba. Ni ukweli kuwa siyo lazima wanajamii wafunzwe kutunza mazingira yao ni jambo walilolifanya tangu enzi.

Ni kweli misitu mingi ambayo wananchi wanailinda kwa njia za mila na desturi za jadi ina miti mingi, mikubwa na minene, ina maji ya chemchemu za asili tena mazingira yanayotamanika, anasema Samira Juma, Ofisa Mkuu Misitu Pemba.

Anapozungumza na Nipashe kwenye makala hii anasema elimu ya kutunza mazingira ni muhimu na matumizi ya mila na desturi kuyalinda ni jambo dhahiri na linaloendelea.

Anasema mila na imani za watu Pemba, zimejengeka kwamba ukiharibu maeneo ya misitu na hifadhi zinazoheshimiwa na jamii kwa matumizi ya kijadi kama matambiko na dua utadhurika kwa namna yoyote ile.

"Utapigwa bakora, utaumwa, utakufa, utapotea, kitatanishi au kuondoka bila kujijua. Hivyo mila hizi zimerithishwa kizazi hadi kizazi na anayekua anajua eneo la msitu fulani haitakiwi kuharibika kwani kuna mapango ambayo hutumiwa kutambika.

Wengine wanatambika kila mwaka na wapo wanaofanya matambiko kwa siku maalum na wote huenda huko kuomba mahitaji kama kuombea wagonjwa, maisha bora na mafanikio," anaongeza Samira.

Anaitaja misitu hiyo kuwa ni pamoja na ile ya Kisiwa Pembe, kilichoko Shehia ya Mtambwe Kusini, kuna msitu mkubwa ambao unatumiwa kufanya mila za kijadi.

Samira anasema hairuhusiwi mwanamke kwenda huko wala yeyote na inapofika saa 6:00 mchana kila aliye ndani anatakiwa uondoke kisiwani mara moja.

Anaongeza kuwa usipofuata masharti hayo unaweza kudhurika na hata sasa msitu uko salama.

Katika Shehia ya Kiuyu kuna msitu ambao ndani yake kuna mapanga ambayo yanatumiwa na wanajamii wa maeneo hayo kijadi.

"Hairuhusiwi kwa mgeni yeyote kwenda peke yake ni lazima afuatane na mwenyeji kuepusha uharibifu wa eneo hilo." Anaongeza Ofisa Misitu Mkuu.

Ukienda kinyume na ukafanya uharibifu wowote utadhurika na hata sasa misitu imehifadhika, anaongeza, Samira.

Anataja msitu wa mikoko wa Kwa Mwanawembe ulioko shehia ya Kiungoni, akisema ni sharti kwenda na mwenyeji ili kuingia na kwamba mgeni akienda peke yake atapotea lengo la kutaka awepo msindikizaji ni kuepusha uharibifu.

Anataja mingine kama misitu ya Matumbini Mwavi Mweusi, kwa Nyundo na kwa Goa Mdiba ambayo iko kisiwa cha Panza kuwa ni minene na miti mikubwa na wananchi wanafahamu kuwa ukienda kichwakichwa unadhurika iwe kuumwa ama kupigwa na watu usiowaona.

Kisiwa N'gombe kilichoko kwenye shehia ya Shumba Mjini anakitaja kuwa kina msitu mnene na kinatumiwa kijadi na kimetunzwa kwa sababu ya kuamini na kuheshimu mila na desturi hasa kudhibiti wasiofahamika kuingia kiholela. Anasema mgeni haruhusiwi kwenda peke yake.

Ipo misitu mingi kama ile ya Kisiwa Mbale, Michi

Zimwi, Kwa Konondo na maeneo ya makaburini kote kumehifadhika. Misitu ni minene na imehifadhika kwa taratibu za kimilia . Yakiwa ni maeneo ya kutambika na kuzika jamaa.

**FAIDA KIJAMII**

"Faida za kutumia mila na desturi ni pamoja na kuleta msukumo katika kulinda na kuhifadhi misitu Pemba na kupata mahitaji ya kijamii kwa urahisi. Wanavuna matunda asilia, mboga, asali, uyoga na dawa. "

Faida nyingine ni kuongeza kipato kwa jamii hasa zinazofuga nyuki kibiashara kwa mfano msitu wa Kiungoni, anasema.

Kubwa jingine Samira anasema ni kuhifadhi vianzio vya maji na chemchem za asili, hasa kwa sababu eneo ni kisiwa na mawimbi ya bahari yanasogea.

"Kuna jingine muhimu ni kuimarisha haiba ya kijani ya kisiwa cha Pemba. Tena kuzuia uharibifu wa visiwa kwani maeneo mengi yamo ndani ya visiwa vidogo vidogo," anasema Samira.

Anasema misitu inaimarisha hali ya hewa na kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi, inazuia pepo za bahari kuingia kwa kasi kubwa katika maeneo ya makazi na mashamba.

"Kwenye misitu ya mikoko ni muhimu inazuia mawimbi ya bahari kuathiri mashamba na makazi. Pia inahifadhi viumbe hai wakiwamo wanyama na ndege, wanaohifadhiwa baharini."

**USHIRIKI WA SERIKALI**

Samira anasema Zanzibar Forest Project, inashirikiana wanajamii kulinda na kuhifadhi maeneo hayo, wakifanya juhudi mbalimbali.

"Mosi tumeanzisha kamati shirikishi za uhifadhi wa misitu ya jamii. Tunashirikiana na kamati hizo kuhifadhi maeneo hayo ambayo yana misitu ya ardhini na mikoko ufukweni."

Aidha, anasema wameanzisha Community Forest Management Agreement (COFMA), ni makubaliano ya usimamizi shirikishi wa misitu baina ya Idara ya Misitu na shehia.

Anasema wanajamii wanatenga maeneo yao kwa mujibu wa matumizi yao na wanatunga sheria ndogo ndogo za kusimamia maeneo hayo ikiwa na pamoja na kugawa misitu kwa matumizi maalum. Anasema yeyote anayevunja sheria hizo adhabu na faini zimeainishwa kwa kila kosa na anaadhibiwa kwa mujibu wa sheria hizo.

Anasema ikishindikana anapelekwa Idara ya Misitu na anaadhibiwa kwa mujibu wa sheria za misitu.

Hata hivyo, anataja changamoto mojawapo kuwa ni baadhi ya maeneo kuwa na ubaguzi kijinsia kwa vile wanawake pekee ndiyo hawaruhusiwi kwenda hivyo wanakosa mahitaji muhimu katika misitu hiyo.

Kwa ujumla anazipongeza jamii, akisema kuwa hata sasa mila na desturi hizo zinaendelea kutumika maeneo mengi na misitu imehifadhika bila ya kutumia nguvu wala gharama.

"Wananchi wa maeneo hayo wanaheshimu mila na desturi zao kutokana na imani na kwa upande wa Idara ya Misitu inashukuru kwa kutumia mila na desturi hizo kwani misitu inaendele kuhifadhika na ridhaa na juhudi za wananchi wenyewe." Anasema Samira.



## Idadi wagonjwa kutoka ughaibuni yaongezeka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

IDADI ya wagonjwa kutoka nje ya nchi wanaokuja kutibiwa nchini imeongezeka kutoka 5,705 mwaka 2022 hadi 7,843 mwaka 2024.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katamba, alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT).

Katambi alisema serikali imeendelea kuhakikisha huduma bora zinaendelea kupatikana katika maeneo ya chini hasa upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa gharama nafuu nchini.

Katambi alisema huduma hizo zimeendelea kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi (Tiba utalii).

"Wagonjwa kutoka nje ya nchi wameongezeka kutoka 5,705 mwaka 2022 hadi 7,843 mwaka 2024. Pia serikali imeendelea kuhakikisha inaongeza vituo vya kutolea huduma za afya vyenye uwezo wa kutoa huduma za dharura za uzazi ikiwamo upasuaji wa kutoa mtoto tumboni kutoka 388 mwaka 2021 hadi 523 mwaka 2024," alisema.

Alisema maendeleo hayo yameleta matokeo makubwa ikiwamo kupungua kwa vifo vya wajawazito kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000.

"Na kupungua kwa vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi kufikia vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000. Namba zinaongea, tumesikia, tumeona na kuthibitisha wenyewe mambo makubwa ambayo yamefanyika ndani ya sekta ya afya chini ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka mitatu tu," alisema Katambi.

Aidha, aliwaomba madaktari na watumishi wa sekta ya afya nchini kuendelea kumuunga mkono Rais Samia ili maono yake ya kuboresha sekta hiyo na wananchi waendelee kupata huduma bora yatimie.

Alisema kupitia mafanikio hayo ni dhahiri kuwa Rais Samia ni kinara wa mageuzi chanya ndani ya sekta ya afya nchini na Afrika.

Alisema Wizara ya Afya imetekeleza programu mbalimbali zinazolenga kutoa mafunzo kazini ikiwamo kwa wakufunzi ngazi ya vituo katika Mkoa wa Kigoma, Tanga, Dar Es Salaam, Mara na Kagera.

Pia, kuendesha mafunzo elekezi kazini kwa huduma za mama na mtoto kupitia programu ijulikanayo kama "Mama Samia Mentorship Program" ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, zaidi ya watoa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto 6,000 wamefikiwa kutoka mikoa yote nchini.

Alisema katika kuimarisha na kuzisogeza huduma za kibingwa na ubingwa bobezi karibu zaidi na wananchi, Wizara imeendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa ngazi hizo kupitia mpango unaojulikana kama Dk. Samia Afya Scholarship wa kutoa ufadhili kwa watumishi wa sekta ya afya kwa utaratibu wa SETI.

# Kamera kudhibiti uhalifu sasa kufungwa mitaani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKOA wa Dodoma umeanza mchakato wa kufunga kamera maalumu za usalama kwenye maeneo ya kimkakati ili kukabiliana na matukio ya kiuhalifu.

Akizungumzia kuhusu mchakato huo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alisema Jiji la Dodoma lina bajeti ya Sh.milioni 300 kuanza kuweka kamera hizo.

"Katika kukabiliana na matukio ya uhalifu mipango iliyopo ni kuanza kuweka CCTV kamera kwenye Mkoa wa Dodoma hasa Jiji ili kuanza kuweka kwenye maeneo ya kimkakati ili kuongeza usalama kwa wananchi wa Dodoma," alisema.

**Katika kukabiliana na matukio ya uhalifu mipango iliyopo ni kuanza kuweka CCTV kamera kwenye Mkoa wa Dodoma hasa Jiji ili kuanza kuweka kwenye maeneo ya kimkakati ili kuongeza usalama kwa wananchi wa Dodoma.**

Aidha, aliagiza maeneo ambayo taa haziwaki zifanyiwe matengenezo na ziwake kama ilivyokusudiwa ili wananchi wawe salama.

"Lengo la taa kuwekwa ni kuongeza usalama kwa wapita njia wengine ambao wanatoka kwenye shughuli zao usiku, sasa wahusika wahakikishe zinawaka kama ilivyokusudiwa ili wananchi wasikumbane na vibaka kwenye maeneo ambayo taa zimewekwa," alisema.

Aliahidi kufuatilia kwa mamlaka zinazohusika na taa za barabara zilizofungwa kwenye mitaa na haziwaki ili zifanyiwe kazi kwa haraka.

Pamoja na mpango huo mapema mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alikutana na kikosi kazi cha miji salama kinachoratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ufungaji wa kamera za kuzuia uhalifu.

Katika mradi huo kamera za awali zitafungwa katika majiji matano ikiwamo Dodoma ili kudhibiti matukio ya uhalifu na wanaokiuka sheria za usalama barabarani.

Masauni alisema kuna baadhi ya nchi zinatumia mfumo huo wa kamera kudhibiti uhalifu na wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa, hivyo wameona waanzishe mradi huo hapa nchini.



Katibu Msaidizi wa Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika, Daniel Eliufoo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha kuhusu mkutano mkuu wa mwaka wa kanda hiyo utakaofanyika jijini humo, kuanzia leo hadi Oktoba 6. **PICHA: BUNGE**

# Waitwa kushiriki mchakato uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** BAHI

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Zaina Mlawa, ametoa wito kwa wananchi wenye sifa kushiriki katika mchakato wa uchaguzi ikiwamo kujiandikisha kwenye Daftari la Wapigakura.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha wadau wa vyama vya siasa na viongozi wa dini kilichofanyika wilayani hapa.

Aidha, alisema kujiandikisha katika orodha ya wapigakura ni hatua muhimu inayompa kila mwananchi mwenye sifa haki ya kisheria kushiriki uchaguzi kama mpigakura au mgombea.

Hivyo, aliwahimiza wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha ili kutumia haki yao ya kupiga kura au kugombea nafasi za uongozi.

Alisema kwa mujibu wa Kanuni ya 27 GN. Na. 571 kampeni za uchanguzi zitaanza Novemba 20 hadi 26 mwaka huu.

"Nitoe wito kwenu wananchi mshiriki katika kugombea nafasi za uongozi ni muhimu katika kukuza demokrasia na kuhakikisha upatikanaji wa viongozi bora kwa maendeleo ya taifa letu," alisema.

Nafasi zitakazogombewa ni Mwenyekiti wa Kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake), wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za wilaya.

Nafasi nyingine ni Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo, Mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake), wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika Mamlaka za Miji.





# Vijana, wanawake wawaangukia wadau wa kahawa mitaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya vijana na wanawake wilayani hapa wamewaomba wadau wa kahawa kuwasaidia kupata mitaji, mashamba na mbegu za kisasa ili waweze kujihusisha na kilimo hicho katika maeneo yao.

Walitoa ombi hilo kwenye mdahalo wa wadau wa kahawa wilayani Mbeya ulioandaliwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Envirocare ambao ulihusisha wadau kutoka bodi ya kahawa, taasisi za kifedha, vyama vya ushirika (Amcos) wakulima kutoka makundi ya wanawake na vijana na wadau wa pembejeo.

**Kupitia vikundi vya wanawake, wamepewa mafunzo ya kulima kahawa na kwamba kwa sasa baadhi yao wanamiliki vitalu vya kuzalisha miche ya zao hilo.**

Mmoja wa vijana walioshiriki kwenye mdahalo huo, Boaz Mpenja, Mkazi wa Kata ya Isuto, alisema hali hiyo inasababisha vijana waone kuwa kilimo cha zao hilo kuwa ni cha wazee peke yao na kulazimika kujiingiza kwenye shughuli nyingine kujiingizia kipato.

Mpenja, alisema zao hilo kwa asili lilikuwa linalimwa na wazee kwa sababu wengi wao walikuwa wanamiliki ardhi kubwa.

Alisema vijana wengi wameamua kujiingiza kwenye shughuli nyingine ikiwamo kuendesha pikipiki za abiria maarufu bodaboda na za magurudumu matatu 'bajaji'.

Alisema tatizo lingine linalochangia vijana wengi wasivutiwe na kilimo hicho ni zao hilo kutumia muda mrefu wakati baadhi yao wanatamani kupata fedha haraka hivyo inawawia vigumu kusubiri miaka miwili hadi mitatu ili miche ikomae na kuanza kuzaa kahawa.

"Sasa hivi vijana wamebadilika wameona kuna fursa kwenye kahawa tofauti na miaka ya nyuma, lakini bado kuna changamoto ya ukosefu wa ardhi, mitaji kwa ajili ya nguvu kazi na kuhudumia mashamba, tunaomba serikali na wadau watusaidie kwa hilo," alisema Mpenja.

David Mwanijembe, alisema zao hilo ni fursa kwa vijana kwa maelezo kuwa hekari moja inaweza kumpatia mkulima zaidi ya Sh. milioni 13 na hivyo kuwa miongoni mwa mazao ambayo yana tija kiuchumi.

Aliiomba serikali kuwasaidia vijana kutatua kero hizo ili wengi wajiingize kwenye uzalishaji na kupunguza tatizo la kuhama kutoka vijijini kwenda mjini.

Meneja mradi wa Shirika la Environcare, Amos Mbwambo, watekelezaji wa mradi wa kuhamasisha kilimo cha zao hilo kwa wanawake na vijana, alisema unatekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma.

Mbwambo, alisema lengo la mradi huo ni kuboresha mnyororo wa thamani wa kahawa nchini ili kuongeza tija na mapato yatokanayo na zao hilo.

Alisema vilevile wanahamasisha wanawake kutumia rasilimali ya ardhi kumiliki uchumi wao ili kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

Alisema kupitia vikundi vya wanawake, wamepewa mafunzo ya kulima kahawa na kwamba kwa sasa baadhi yao wanamiliki vitalu vya kuzalisha miche ya zao hilo.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda, alisema kahawa ni zao la kimkakati katika wilaya hiyo na linalimwa kata 10.

Mapunda, alisema serikali inaendelea na mikakati ya kuhakikisha wankulima wanapata pembejeo.



Wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa wa ngazi ya kata na mitaa katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wakila kiapo cha uaminifu wakati wa uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima walalamikia bei ya pareto

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

OFISI ya Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mbeya imeagizwa kukutana na wadau wa pareto kupanga bei yenye tija kwa wakulima wa zao hilo, ili kuwainua kiuchumi.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera wakati wa ziara ya kusikiliza kero za wananchi katika Halmashauri ya Mbeya baada ya baadhi ya wakulima kudai bei ya pareto ya sasa Sh. 3,200 hadi 3,500 haiwanufaishi kulingana na gharama wanazotumia kuendesha kilimo hicho.

Homera, alisema uzalishaji wa zao hilo umeongezeka kutoka tani 2,000 hadi 4,000, hivyo ni muhimu wadau hao, ikiwamo Bodi ya Pareto kuongeza bei kama ilivyofanyika kwa mazao mengine ili wakulima wa zao hilo wapate tija inayoendana na malengo yao.

"Zao la pareto lina kazi kubwa, kwanza mpaka kufikisha kilo moja ni changamoto kubwa kama tumeweza kuongeza bei ya kakao kutoka Sh. 4,000 hadi Sh.32,000 na tumbaku kwa sasa inauzwa hadi Sh. 8,000 sasa tunakwenda kuhakikisha na bei ya pareto inapanda ili wakulima wanufaike," alisema.

Alisema hatua hiyo ni muhimu kwa wakulima wa Mbeya Vijijini kwani ndio wilaya inayoongoza kwa uzalishaji wa pareto.

Alisema ili kuendeleza tija ya zao hilo, msimu uliopita Serikali ilitoa zaidi ya Sh.milioni 200 kwa ajili ya kuanzisha vitalu vya mbegu bora ambazo ziligawiwa kwa wakulima.

Vilevile, alisema wamejenga viwanda sita ndani ya mkoa huo kwa ajili ya kuongeza thamani ya zao hilo na kutaka wakulima hao kutokata tamaa na changamoto zinazojitokeza kwani serikali inaendelea kufanya juhudi kuhakikisha wanaongeza tija ya uzalishaji.

Homera, aliwataka wakulima kuacha kuchuma maua ambayo hayajakomaa ili kuondokana na changamoto ya soko duniani na kuwakataa walanguzi ambao huwarubuni kwa maslahi yao binafsi.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo, Tito Mashaka, alisema wanakata tamaa ya kuendelea na kilimo hicho kwa maelezo kwa kuwa bei imekuwa haiongezeki.

Mashaka, alisema wakulima wamekuwa wakipangiwa bei miaka yote bila wao kushirikishwa na kuwafanya wajione kuwa wao hawana maamuzi ya bei ya zao hilo.

## Viongozi wa siasa wapewa neno

**Na Mwandishi Wetu,** CHUNYA

VIONGOZI wa vyama vya siasa wilayani hapa Mkoa wa Mbeya wametakiwa kutoa ushirikiano ili kuhakikisha uchaguzi wa serikali za mitaa unafanyika kwa amani na utulivu.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Tamim Kambona, kwenye mkutano na makundi kwa ajili ya kutoa maelekezo kuhusu uchaguzi huo utakaofanyika nchini Novemba 27, mwaka huu.

Kambona, alisema katika uchaguzi huo hakuna mgombea atakayepita bila kupingwa bali kila mmoja atapaswa kupigiwa kura kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa.

Alisema wapigakura, wagombea na wadau wa uchaguzi wanapaswa kupata maelekezo kuhusu utaratibu wa uchaguzi huo utakavyofanyika kuanzia kujiandikisha mpaka kupiga kura.

"Maelekezo yote muhimu yatawekwa ili wagombea na wapigakura wayajue na kufuata ili kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa haki na uwazi na kwa kuzingatia sheria zilizowekwa," alisema Kambona.

Akitoa salamu za serikali, Mkuu wa Wilaya hiyo, Mbarak Batenga, alisema katika uchaguzi huo wilaya inapaswa kuwa mfano wa kuigwa kwa kufanya siasa safi na kudumisha amani.



# INEC yaja kivingine uboreshaji taarifa wapigakura kwa simu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi imesema imeboresha mfumo wa uandikishaji ambao kwa sasa utamwezesha mpigakura kufanya maboresho ya taarifa zake kwa kutumia simu ya kiganjani au kompyuta.

Mjumbe wa tume hiyo ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Abdallah Omar, alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa tume hiyo kwa wadau wa uchaguzi.

Alisema wanaotumia simu zisizo janja nao wanaweza kutumia huduma hiyo na kupata maelekezo pamoja na taarifa zao.

Alisema mzunguko wa sita wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura unatarajiwa kuanza Oktoba saba hadi 13, mwaka huu kwa visiwa vya Unguja na Pemba.

"Uboreshaji huu kama ilivyokuwa wa mwaka 2015 na 2020 utahusisha matumizi ya teknolojia ambapo hutumika katika kumtambua mtu na kumtofautisha na mwingine. Unahusisha uchukuaji wa alama za vidole vya mikono, picha na saini na kuhifadhiwa kwenye kanzidata ya wapigakura," alisema Jaji Asina.

Alisema uboreshaji huo ni tofauti na wa miaka iliyopita ambapo kwa mwaka huu utatumia teknolojia ya BVR kits zilizoboreshwa kwa kuwekewa programu endeshi ya kisasa zaidi.

Aidha, alisema kujiandikisha kuwa mpigakura zaidi ya mara moja ni kosa la kisheria kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 114(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Namba 1 ya mwaka 2024.

Alisema kifungo hicho kinaeleza kuwa mtu yeyote atakayeomba kuandikishwa zaidi ya mara moja atakuwa ametenda kosa la kisheria na akikutwa hatiani adhabu yake ni faini isiyopunguwa Sh. 10,0000 na isiyozidi Sh. 30,0000 au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopunguwa miezi sita na kisichozidi miaka miwili gerezani au vyote kwa pamoja.

Alisema tume imeweka utaratibu kwa watu wenye ulemavu, wazee, wagonjwa, wajawazito na kinamama wenye watoto wachanga watakaokwenda vituoni kupewa fursa ya kuhudumiwa bila kupanga foleni.

Hivyo, aliwataka wadau wa uchaguzi kuwafahamisha wananchi wenye sifa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha au kuboresha taarifa zao vituoni kwa kuwa utaratibu mzuri wa kuwahudumia umewekwa.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa tume hiyo, Kailima Ramadhani, alisema uboreshaji wa taarifa nchini unatarajia kukamilika Machi mwakani.

Alisema itahusisha mambo mbalimbali ikiwamo kutoa kadi mpya, waliopoteza kadi au kadi kuharibika, kuondoa wapigakura waliokosa sifa kutokana na sababu mbalimbali.

Aidha alisema wapigakura 5,586,433 wapya wanatarajiwa kuandikishwa sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699 waliopo kwenye daftari.




Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Omari, akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa wadau wa uchaguzi katika kisiwa cha Unguja, Zanzibar jana. **PICHA: INEC**

## Serikali yapeleka umeme Bonde la Mbuyu Joda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaib Hassan Kaduara, amesema uwekezaji mkubwa wa huduma ya umeme katika Bonde la Mbuyu Joda Wilaya ya Wete Pemba, unalenga kuwakomboa wananchi kiuchumi kupitia shughuli za kilimo.

Alisema serikali imefanya juhudi mbalimbali katika kuwakomboa wananchi kiuchumi na ndiyo maana wizara imepeleka umeme katika bonde hilo ili iwasaidie katika shughuli za kilimo.

Alisema hayo wakati akikagua mradi wa usambazaji umeme katika mashamba hayo.

Hivyo, aliwataka wakulima kuitumia fursa hiyo kuzalisha bidhaa kwa wingi na zenye ubora, ili ziwepo nyingi sokoni na wananchi wapate unafuu.

"Huu ni uwekezaji mkubwa tulioufanya hapa, mjipange vizuri katika uzalishaji ili serikali ipate kuwaunga mkono zaidi, hii itasaidia kuzalisha bidhaa kwa wingi na kupata kipato kitakachotusaidia katika maisha yenu ya kila siku," alisema.

Aidha alisema ni lazima kwa wakulima hao wakubali kubadilika kwa ajili ya maendeleo pamoja na kufanya utafiti wa kitaalamu, kutumia dawa na mbolea ili wazalishe bidhaa zenye ubora.

"Tutakaa na Wizara ya Kilimo ili tusaidie nguvu za pamoja kuboresha miundombinu mbalimbali itakayowasaidia kwenye kilimo, kwa sababu ukiwakomboa wananchi ni sawa na kuikomboa nchi," alisema.

Wananchi wa bonde hilo waliishukuru serikali kupitia kusema huduma hiyo ya umeme itawapunguzia matumizi ya petroli ambayo wanaitumia kupandishia maji pindi wanapomwagilia mazao yao.

Mmoja wa wananchi hao, Ali Msanif Ali alisema: "Gharama zitapungua kwa kiasi kikubwa kwa sababu lita tano za mafuta ya petroli ni Sh. 15,000 tunazitumia kwa mara moja tu kumwagilia maji, jambo ambalo linatusababishia hasara kubwa, lakini kuja kwa umeme tunaamini itaturahisishia".

Jamal Juma Kombo alisema wamejipanga katika kuhakikisha wanajiimarisha katika kilimo na kuiomba serikali kuwaboreshea mabwawa yao kwa ajili ya ufugaji.

"Tunaomba baada ya mradi huu kukamilika tukopeshwe mita na pia tupewe mkopo wa fedha ili tupate mtaji utakaotusaidia katika shughuli zetu za kilimo, kwa sababu huku Makaani kilimo kinakubali sana mazao tofauti tofauti," alisema.

Mradi huo umegharimu Sh. milioni 289, unahusisha njia kuu ya umeme yenye urefu wa kilomita nne, ujenzi wa njia ndogo ya kilomita nane na uwekaji wa vituo vinne vya trasfoma.

## Waziri: Watuhumiwa matukio ukatili semeni ukweli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Riziki Pembe Juma, amewataka wananchi wanaotuhumiwa na makosa ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia watoe taarifa sahihi na siyo taarifa za uongo.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir.

Ameir alitaka kujua wanaume wengi wamejikuta wakipata hatia ya kuhukumiwa jela kutokana na kesi nyingi za kusingiziwa kubaka.

Akijibu swali hilo, Waziri Pembe alisema haki bila ya uwazi na bila uwajibikaji wa misingi ya kisheria haipatikani, hivyo ni vyema wananchi wote wasimamie haki.

Alisema wizara yake inatumia utaratibu wa kufuatilia matukio ya ukatili na udhalilishaji kwa wanaume ambao wamesingiziwa kesi kwa kutumia utaratibu wa kisheria bila ya kuingilia kazi za muhimili mwingine.

Alisema pia wanatumia utaratibu wa kutoa elimu ya dhana ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, ili kujikinga na kuripoti matukio ya udhalilishaji kwa jamii na watuhumiwa.

"Wizara yangu inatambua juu ya umuhimu wa mgawanyo wa madaraka ila bado haipendezewi na uwepo wa uvunjifu wa haki za watu. Kwa kuwa msingi wa haki unajengwa kwa uwazi, ukweli na usawa kama ilivyoelekezwa katika Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984," alisema.

Aidha, alisema stahiki anayopatiwa mtuhumiwa baada ya kutolewa hukumu na kubainika kuwa hakutendewa haki ni kukata rufani na kuomba kufanyiwa mapitio ya taratibu za kisheria kwa makosa yaliyowasilishwa mahakamani.

Alisema hilo hufanyika ili kulinda uhuru wa mahakama na siyo kuingilia kazi za mahakama, kwamba wizara kwa kutumia wataalamu wa saikolojia na masuala ya kijamii hutoa ushauri nasaha kwa mtuhumiwa ili kutuliza joto na kumpa moyo wa kutambua misingi ya upatikanaji wa haki.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**BASIL NORBERT WILLA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1601-0012 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TENGERU BOYS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:**PHQ/DAR/UBU/210881/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**REHEMA DAUDI SINAWIU** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S3907/0047** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIBAHA GIRL'S SECONDARY** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. **9910842521702.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**RAKESH BABU TULSIDAS** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 358 BGU na MC 521 BFX.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/211078/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KAMUGISHA SABASI RUFULENGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T818DEN** aina ya Toyota BELTA , Chassis No. **SCP921021838,** Engine No. **2SZ6540138.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/DOD/43527/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**CHRISTOPHER RAPHAELI MNGARA**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 984 DRF** Chasses Namba **L7GPCKLY5N1011342,** Engine Namba **KL16FMJN5011342** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taarifa :
**PHQ/ KIL/ SAM/10257/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISAYA CHARLES** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **LION KING y**enye usajili namba **MC 203 AQR** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI CONTROL NAMBA:
**9910842499136**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU DINNAH NAFTAL** NKWERA anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T465BRR** aina ya **NOAH** Rangi Pearly White.Kwa yeyote atakayefanikiwa kuiona kadi hiyo atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu naye. Taarifa ya Polisi namba
**PHQ/DOD/DOD/43420/2024**

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIBONDO**

**MAHALI: KIBONDO**

**MAOMBI NA 2 MWAKA 2024**

**GERSHON BILONKERA NTEGANYA..............MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**NGARAMA NTENDERI NTEGUYE, BANYANKA MAKALIUS NA PASIKALI MATATA...........................................WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: NGARAMA NTENDERI NTEGUYE, BANYANKA MAKALIUS NA PASIKALI MATATA POPOTE MLIPO**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 22 mwezi 10 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe F. CHINUKU Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/ muhuri wa Baraza hili leo tarehe 14 mwezi 8 mwaka 2024

CHAIRMAN DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL KIBONDO TANZANIA

MWENYEKITI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 19261/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late JUNIOR EMMANUEL NYAMWINO of Nzuguni A Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY HELLEN RICHARD JUMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 26 Day of 9, 2024
Presented for filing this 23 day of 08, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 317 .... La 2024**

**RENATUS JOSEPH NYALALI ................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**(1) CECY MICHAEL YASIN**
**(2) GIBONS JOSEPH MWAIGONELA...........MDAIWA/WADAIWA**
**(3) MSOLOPA INVESTMENT CO LTD**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**(4) CECY MICHAEL YASIN**
**(5) GIBONS JOSEPH MWAIGONELA**
**(6) MSOLOPA INVESTMENT CO LTD**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**RENATUS JOSEPH NYALALI** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwanyamala ) . shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 03/10/2024 saa 03: 00 asubuhi/ mchana mbele ya J.W. SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 03 Mwezi 09 ...2024

MWENYEKITI

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa : GEITA**

**Shauri la madai Na: 139/2024**

**Jina la Mdai: MICHAEL ZEPHANIA LUDIGIJA**

**Jina la Mdaiwa: JOSEPH KITULA & MWENZAKE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: JOSEPH KITULA**
**GEITA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba "Namdai mdaiwa Tsh. 4,500,000/=)**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 04 mwezi 10 mwaka 2024 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26 mwezi 09 mwaka

HAKIMU RESIDENT MAGISTRATE GEITA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 149 YA 2024**

**TAFUTA ABDALLAH MILONDOMO.........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**1. JIDAI MAONA**
**2. LWENGE MZILE........................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA LWENGE MZILE**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 31/10/2024 mbele ya Mwenyekiti E. MOGASA wewe mwenyewe au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 27 mwezi Septemba, 2024.

**E. MOGASA**
**MWENYEKITI.**

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042 DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wanaigeria kufanya maandamano leo

**ABUJA, Nigeria**

BAADHI ya raia wa Nigeria wameonyesha nia yao ya kufanya maandamano leo, Oktoba 1, wakati taifa hilo la Afrika Magharibi litakapokuwa likiadhimisha miaka 64 ya uhuru wake.

Waandalizi wa maandamano hayo walisema jana kuwa maandamano hayo, yaliyopewa jina la (#FearlessOctober1), yatafanyika kote nchini humo kushinikiza kurejeshwa kwa ruzuku ya mafuta, na pia kushughulikia masuala mengine ya umma.

Juwon Sanyaolu, mratibu wa kitaifa wa vuguvugu la vijana wa Nigeria, alisema kwamba polisi wamefahamishwa kuhusu maandamano yaliyopangwa kama inavyotakiwa na sheria.

„Tumemwandikia inspekta mkuu wa polisi kumfahamisha kuhusu maeneo yetu ya maandamano,“ Sanyaolu alisema, kama alivyonukuliwa na gazeti la Punch la Nigeria.

Waandalizi wa maandamano hayo walisema yatakutana katika uwanja wa Eagle Square katika mji mkuu wa Abuja, na chini ya daraja la Ikeja katika jiji la kibiashara la Lagos.

Inspekta Jenerali wa Polisi wa Nigeria, Kayode Egbetokun, aliamuru kutumwa kwa maofisa wa polisi katika vituo vya kimkakati vya serikali ili kuwalinda dhidi ya uharibifu unaoweza kujitokeza.

Egbetokun pia amewasisitiza wanaopanga maandamano hayo kubatilisha uamuzi wao, bila kutoa sababu ya hilo.

Waandalizi wa maandamano hayo walisema maombi yao ya awali kwa serikali kuhusu kupunguza matatizo ya kiuchumi hayakusikilizwa, na hivyo kusababisha wimbi jipya la hatua za mitaani.

Aidha, ilielezwa kuwa kwa sasa Nigeria inapambana na janga la gharama ya maisha linalosababishwa na mfumuko wa bei, naira iliyoshuka thamani, na kuondolewa kwa ruzuku ya mafuta.

Naye Rais wa taifa hilo, Bola Tinubu, aliwataka Wanigeria kuwa na subira na sera za kiuchumi za utawala wake akisema hivi karibuni zitazaa matunda.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, takriban Wanigeria milioni 25 wanakabiliwa na tisho la njaa.

Pia ilielezwa kuwa ukosefu wa usalama pia unabaki kuwa changamoto kubwa kwa serikali ya Rais Tinubu, huku utekaji nyara kwa ajili ya fidia na mashambulizi ya waasi yakiongezeka.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa wakati wa maandamano ya hivi karibuni yaliyofanyika nchini Nigeria mapema mwezi Agosti, takriban watu 13 waliuawa, huku shirika la Amnesty International likikadiria idadi ya waliofariki kuwa zaidi ya 21.

Vile vile, ilielezwa kuwa mamia ya watu walikamatwa wakati wa maandamano hayo, huku wengi wao sasa wakikabiliwa na hatua za kisheria.

***TRT***



Raia waliokimbia machafuko Lebanon wakisubiri kuvuka mpaka kuingia Syria, juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Kimbunga chasababisha vifo 11 Marekani

**NORTH CAROLINA, Marekani**

MAJIMBO ya Kusini Mashariki mwa Marekani yanaendelea kukabiliana na vifo pamoja na ukosefu wa vifaa muhimu kwenye maeneo ya ndani, huku nyumba zikiharibiwa kutokana na kimbunga Helene, ambacho maofisa wamesema kitakuwa na athari kubwa.

Gavana wa North Carolina, Roy Cooper, alisema jana kwamba idadi ya vifo kwenye jimbo hilo imefika 11, wakati ikitarajiwa kuongezeka, huku timu za uokozi zikijitahidi kufikia maeneo ya ndani, yaliyokumbwa na mafuriko pamoja na kuharibika kwa miundombinu kama barabara.

Jimboni Florida na hasa kwenye kaunti ya Big Bend, wakazi wameripotiwa kupoteza karibu kila kitu, huku asilimia 97 wakiwa hawana umeme kutokana na kimbunga hicho.

Rais wa Marekani, Joe Biden, alisema uharibifu wa Helene umekuwa mkubwa huku akiahidi msaada wa serikali kuu kwenye majimbo yaliyoathiriwa.

Helen ni kimbunga cha nane kutoka bahari ya Atlantic kupiga Marekani kwenye msimu huu wa vimbunga ulioanza Juni.

***VOA***

**Jimboni Florida na hasa kwenye kaunti ya Big Bend, wakazi wameripotiwa kupoteza karibu kila kitu, huku asilimia 97 wakiwa hawana umeme kutokana na kimbunga hicho.**

# Hezbollah yasema iko tayari kwa lolote

**BEIRUT, Lebanon**

NAIBU mkuu wa kundi la Hezbollah Sheikh Naim Qassem, amesema wako tayari kwa lolote katika kukabiliana na Israel, ikiwa ni kauli ya kwanza ya kiongozi huyo tangu shambulio la Israel lilipomuua mkuu wa kundi hilo, Hassan Nasrallah, ambaye bado haijulikani lini atazikwa.

Katika hotuba yake aliyoitoa jana Qaseem alisema wako tayari kwa lolote hata kwa mapambano ya ardhini na vikosi vya Israel na kwamba wataendeleza mwongozo ulioachwa na Nassrallah katika vita hivyo.

Aidha, Iran ambayo ndiyo mfadhili mkuu wa Hamas na Hezbollah, ilisema inafuatilia kwa karibu yanayoendelea.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Iran, Nasser Kanaani, alisema Tehran haitoacha vitendo vya uhalifu vya Israel bila kujibiwa, akimaanisha mauaji ya viongozi waandamizi wa Hezbollah nchini Lebanon.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean Noel Barrot yuko Beirut akiwa ni mwanadiplomasia wa kwanza wa kigeni wa ngazi za juu kuitembelea Lebanon hivi sasa tangu Israel ilipoanzisha mashambulizi, akisisitiza Israel isitishe mashambulizi hayo.

Mbali na miito ya kimataifa ya kutaka kutoutanua mzozo huu wa Mashariki ya Kati, Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu, Sheikh Mohamed bin Zayed Al Nahyan, aliahidi kutoa msaada wa dharura wa dola milioni 100 kwa Lebanon.

Pia Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya (EU), Josep Borrell, aliitisha mkutano wa dharura wa mawaziri wa umoja huo ili kujadili hali inayozidi kuwa tete nchini Lebanon.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Filippo Grandi ambaye ni Kamishna Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Wakimbizi (UNHCR). Abbas Dalloul raia wa Lebanon aliyekimbilia Syria, watu zaidi ya 100,000 wamelazimika kuondoka Lebanon na kukimbilia nchini Syria.

"Hatujawahi kushuhudia vita kama hivi, kwa vurugu na uharibifu. Hatukuona uharibifu wa aina hii mwaka 2006 wakati wa mashambulizi ya anga. Kijiji chetu hakikushambuliwa mwaka 2006. Lakini, vita hivi ni vya kikatili kwa vijiji jirani na nyumba zetu. Baada ya siku tatu, watoto walikuwa na hofu," alisema.

Wakati hayo yakielezwa, Israel iliendelea kuyalenga maeneo kadhaa ya kundi la Hezbollah ndani ya Lebanon, huku kukiwa na ripoti kuwa jengo moja la ghorofa limeshambuliwa kwa makombora katikati mwa mji mkuu Beirut. Mamlaka za Lebanon zikisema zaidi ya watu 100 wameuawa katika kipindi cha saa 24 zilizopita. Katika hatua nyingine, kundi la wanamgambo wa Kipalestina la Hamas lilisema kuwa kiongozi wake nchini Lebanon, Fatah Sharif, ameuawa pamoja na maofisa wengine wawili katika shambulio la anga la Israel kusini mwa nchi hiyo.

Wizara ya Afya ya Lebanon ilisema zaidi ya watu 1,000 wameouawa na wengine 6,000 wamejeruhiwa kufuatia wiki mbili za mashambulizi ya Israel.

# Kikundi cha sanaa St Peter Claver chafunika mahafali kidato cha nne

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KIKUNDI cha sanaa cha wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya St Peter Claver ya jijini hapa mwishoni mwa wiki walikuwa kivutio kwenye mahafali ya 11 ya kidato cha nne shuleni hapo.

Katika mahafali hayo kikundi hicho kilionyesha umahiri kwenye mchezo wa sarakasi, ngoma za asili pamoja na umahiri wa kuimba nyimbo mbalimbali za hamasa.

Akizungumza kwenye mahafali hayo, mkuu wa shule hiyo, Padre Kalongo Bubelwa, alisema Shule ya St Peter Claver mbali na umahiri kwenye elimu, pia wako vizuri katika michezo mbalimbali.

Alisema wamekuwa wakifanya vizuri kwenye michezo ya mpira wa miguu, netiboli, sarakasi pamoja na kwaya zinazoundwa na wanafunzi.

"Niwasihi wanafunzi wanapohitimu masomo yao, wasipoteze vipaji vyao, wakaviendeleze huko waendako na nina uhakika vitawasaidia," alisema Padri Kalongo.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa wanafunzi kushiriki katika michezo mbalimbali kwa kuwa licha ya kuwajenga kiafya, lakini pia inawapa nafasi ya kufanya vizuri kwenye masomo yao.

„Michezo imekuwa ikiwasaidia sana wanafunzi kujiweka sawa na masomo yao, hapa shuleni, tumetenga siku kwa ajili ya michezo tu kwa wanafunzi," alisema.

# LEMA: HATUIHOFII SIMBA QUEENS

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Wanawake, Yanga Princess, Edna Lema, amesema hawaihofii hata kidogo Simba Queens katika mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii utakaochezwa kesho, licha ya kwamba huwa hawana matokeo mazuri wanapokutana nayo.

Akizungumza akiwa kwenye maandalizi ya mchezo huo utakaopigwa, Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam, Lema, alisema wamejipanga kisawasawa kupambana na wapinzani wao hao japo kwa sasa wana wachezaji wengi wapya na wanaendelea kuijenga timu, lakini hawatokuwa wanyonge tena mbele ya mabingwa hao watetezi wa Ligi ya Wanawake.

„Tunafahamu kuwa kwa sasa tunajenga timu mpya na tupo kwenye maandalizi kupambana na Simba Queens, ni timu kubwa, ina uzoefu katika michezo ya kimataifa, ina wachezaji wazuri ambao wamekaa muda mrefu, tunafahamu pia kuwa hatujapata matokeo mazuri katika mechi za karibuni, lakini hiyo siyo sababu ya kutokujiandaa na mchezo huo, tumeajiandaa vyema sababu safari hii na hatukokuwa wanyonge tena," alisema Lema.

Hata hivyo alisema wataingia uwanjani kwa heshima zote kwa wapinzani wao kwani wanatambua ubora wao, lakini hiyo haimaanishi kuwa matokeo yatakuwa kama watu wanavyofikiria.

"Mimi sina presha sana na mchezo huo kwani inawezekana mimi ndiyo kocha niliyecheza dabi nyingi kama tano au sita hivi, siogopi mechi kwa sababu eti ni timu kubwa tunayokwenda kucheza nayo, hizi ndiyo mechi ambazo zinanijenga mimi, ingawa dabi siku zote huwezi kuitabiri nje ya kiwanja, lakini ukisema wachezaji wangu wanaiogopa Simba Queens, au mimi naogopa mechi kubwa si kweli," alisema.

Timu hizo zinakutana huku Simba Queens ikiwa na rekodi nzuri ya ushindi dhidi ya wapinzani wao.

Kabla ya mechi hiyo ya dabi, kutakuwa na mchezo kati ya JKT Queens dhidi ya Ceasiaa Queens, na washindi wa mechi hizo mbili watakutana fainali Jumamosi ijayo ambapo kabla ya hapo kutakuwa na mchezo wa kusaka mshindi wa tatu.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya St Peter Claver ya jijini Dodoma, wakiwa wamevalia vazi la asili la Kimasai, wakati wakiimba na kucheza ngoma ya kabila hilo katika mahafali ya 11 ya kidato cha nne mwishoni mwa wiki. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Malindi SC yatetea matokeo ya sare

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa Malindi SC, Suleiman Mohamed, amesema matokeo ya sare waliyoyapata kwenye mchezo uliopita hayamaanishi kuwa timu hiyo imeanza kupunguza kasi yake kwenye michezo ya Ligi Kuu Zanzibar.

Malindi SC juzi ililazimishwa sare ya bao 1-1 na wapinzani wao wa muda mrefu Mlandage FC katika michezo wao wa ‚Dabi' ikiwa ni mwendelezo wa Ligi Kuu ya Zanzibar inayodhaminiwa na PBZ.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika mchezo huo juzi, kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Mohamed alisema mchezo wowote wa dabi unakuwa mgumu kutokana na presha yake.

Alisema timu yake haikucheza vizuri kama ilivyozoeleka na imetokana na hofu ya mchezo wenyewe na wachezaji wake walikosa nafasi nyingi za wazi hasa katika kipindi cha pili.

"Ulikuwa mchezo muhimu lakini hatukupata matokeo tuliyoyatarajia tumegawana alama, safu yangu ya ushambuliaji haikuwa bora," alisema Mohamed.

Kwa upande wake, Kocha wa Mlandege FC, Hassan Ramadhani, alisema timu yake ilicheza vizuri kwa upande wa ulinzi kwa kudhibiti mashambulizi ya wapinzani wao.

Alisema safu ya ushambuliaji haikufanya vizuri licha ya kufanikiwa mara nyingi kuingia katika eneo la hatari la wapinzani wao.

"Bado sijajua wachezaji wamepatwa na nini, mara kadhaa tunashambulia na kutengeneza nafasi, lakini bahati mbaya tumeshindwa kupachika mabao," alisema.

Kwa matokeo hayo Mlandege FC imefikisha pointi sita na kushika nafasi ya sita kwenye msimamo wakati Malindi SC ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba na imecheza michezo mitatu.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ALLEGRI ATAJWA MAN

KLABU ya Manchester United inamfikiria kocha wa zamani wa Juventus Massimiliano Allegri kama uwezekano wa kuchukua nafasi ya Erik ten Hag. ***(Caught Offside)***

### PATTERSON AWANIWA

MANCHESTER United wanafikiria kumsajili mlinda mlango wa Sunderland, Anthony Patterson mwenye umri wa miaka 24 kuwa msaidizi wa Andre Onana. ***(Sun)***

### ZUBIMENDI ATAKIWA CITY

MANCHESTER City wanafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Insider)***

### BECKER ANYATIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inafuatilia matukio kuhusu mlinda mlango wa Liverpool na Brazil, Alisson Becker mwenye umri wa miaka 31, ambaye amekuwa akihusishwa na uhamisho wa Saudi Arabia. ***{Sun)***

### DAVID AWINDWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inaweza kuwapa changamoto Inter Milan na Juventus kwa ajili ya kumsajili fowadi wa Lille kutoka Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24. ***(Calciomercato)***

### SANCHEZ KWENYE RADA ZA LIVERPOOL

LIVERPOOL ni moja ya klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazofuatilia hali ya winga wa Sevilla raia wa Hispania, Juanlu Sanchez mwenye umri wa miaka 21. ***(Caught-Offside)***

### BARELLA BEI JUU

MANCHESTER City wameambiwa watalazimika kulipa angalau pauni milioni 70 ili kumsajili kiungo wa kati wa Italia, Nicolo Barella mwenye umri wa miaka 27 kutoka Inter Milan. ***(Football Insider)***

### CHILWELL KUUZWA

CHELSEA itahimiza ombi la Januari la kumuuza beki wa kushoto wa England, Ben Chilwell - licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kurejea kwenye kikosi chao cha kwanza. ***(Mirror)***


### LIVERPOOL HAINA WASIWASI

LIVERPOOL hawana wasiwasi na madai kuwa mshambuliaji mpya wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32, tayari amekubali kujiunga na klabu ya Saudi Arabia mkataba wake utakapokamilika msimu ujao. ***(Football Insider)***

### SZCZESNY KUTUA BARCELONA

BARCELONA wamepewa ruhusa na LaLiga kumsajili mchezaji huru Wojciech Szczesny mwenye umri wa miaka 34 - kipa wa zamani wa Poland, Arsenal na Juventus - kama mbadala wa kipa wa Ujerumani ambaye ni majeruhi, Marc-Andre ter Stegen, 32. ***(Mundo Deportivo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG ALIA NA WACHEZAJI WAKE MANCHESTER UNITED

**Asema hawachezi kwa kujituma na wamekosa imani...**

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag alilaumu ukosefu wa 'imani' baada ya timu yake kuchapwa 3-0 nyumbani na Tottenham Hotspur katika mchezo wa Ligi Kuu England juzi.

Kikosi cha Kocha Ange Postecoglou kilikuwa na mchezo mzuri pale Old Trafford, ambapo wenyeji walilazimika kucheza kipindi cha pili pungufu baada ya Bruno Fernandes kutolewa nje kwa kadi nyekundu.

Tottenham walipata bao la kuongoza ndani ya dakika tatu wakati Micky van de Ven alipokimbia kwa umbali wa yadi 70 kupitia eneo la kiungo la United na safu ya ulinzi kabla ya kumpiga chenga Brennan Johnson na kupachika bao.

Akizungumza na BBC Sport baada ya mchezo huo, Ten Hag alikosoa molari ya wachezaji wake.

"Kuruhusu bao baada ya dakika mbili au tatu kama hizo, ilifanya kitu kwa imani yetu," alisema.

"Sio lazima kabisa. Kuruhusu bao kama hili, kiungo mpinzani wa kati anaingia na kuipita timu nzima upande wa kulia na kisha winga na kufunga bao. Kosa lile lile la katikati ya wiki dhidi ya Twente, linapaswa kusimamishwa katika dakika ya kwanza.

"Kuanzia wakati huo na kuendelea tulikuwa na mkazo kwenye mpira. Hatukuweza kupata pembetatu, tulikuwa na wakati mzuri, lakini kutoka wakati huo hatukuweza kupata nafasi. Na tunaweza kufanya vizuri zaidi kuliko hapo.

"Tulipata nafasi na muda wetu wa kurejea mchezoni na Joshua Zirkzee na Alejandro Garnacho tukiwa bado na wachezaji 11 na baada ya kadi nyekundu pia tukawa na muda.

"Tulipata nafasi zetu kabla ya kipindi cha mapumziko na kipindi cha pili tukiwa na wachezaji 10 tulipata nafasi pia.

"Kwanza tunapaswa kukabiliana na hili na kuonyesha uthabiti. Hii haitoshi. Inabidi tukubali hili na kuwa bora zaidi. Tuzingatie mchezo unaofuata na kufanya mambo vizuri zaidi kuliko tulivyofanya leo."

# DE JONG AVUNJA UKIMYA WA MSHAHARA



**BARCELONA,** HISPANIA

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Frenkie de Jong amekanusha madai anapokea kiasi cha euro milioni 37 kwa mwaka.

Wakati De Jong akiwa Katalunya, imethibitika kuwa na misukosuko katika miaka michache iliyopita.

Amekaa nje ya dimba kwa miezi mitano iliyopita kutokana na jeraha tata la kifundo cha mguu na ripoti zimedai kuwa alikataa matakwa ya klabu kufanyiwa upasuaji wa tatizo hilo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mara kwa mara amejikuta katika rada za uhamisho, huku Barcelona mara nyingi ikisemekana kuwa tayari kumuuza ili kuondoka na bili ya mshahara wake mkubwa.

Alikuwa akivutiwa sana na Manchester United mnamo 2022 wakati bosi wake wa zamani wa Ajax, Erik ten Hag alipoteuliwa kuwa kocha wao mpya, ingawa uhamisho haukutimia.

Katika mahojiano na Barcelona One, De Jong alijibu kuhusu maisha yake ya kitaaluma na kutaka kuelezea upande wake.

"Ninaelewa kufadhaika kwa sababu katika kipindi chote cha kuwa majeruhi nimechagua kukaa kimya," alisema De Jong.

"Lakini mambo yanaibuka ambayo si ya kweli, kama vile sitaki upasuaji, kwamba ninapata fedha nyingi, kama euro milioni 37. Hiyo sio kweli.

"Halafu watu wanazungumza sana kama nifanyiwe upasuaji. Sio kweli kwamba klabu ilinIambia nifanyiwe upasuaji na sikutaka.

"Kila mtu katika klabu, madaktari na mimi sote tulikubali kwamba upasuaji haukuwa chaguo bora. Imekuwa inasikitisha sana kwa mchezaji anayeishi na kupumua soka kuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu."

## Flick akerwa na kipigo

**BARCELONA,** HISPANIA

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Hansi Flick alilaumu sana timu yake kwa kufungwa mabao 4-2 na Osasuna Jumamosi usiku.

Mwanzo mzuri wa Barca katika msimu mpya wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, ulimalizika kwa kufungwa huko Pamplona, na uamuzi wa Flick kufanya mabadiliko matano kwenye kikosi chake cha kwanza ukitiliwa shaka.

Lamine Yamal na Raphinha walikuwa miongoni mwa wachezaji walioachwa kwenye benchi kwa matumaini ya kukiweka kikosi safi, lakini uamuzi huu uliambulia patupu na Barcelona wakapata pigo kubwa.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari, Flick alielezea uamuzi wake wa kubadilisha timu na kuchukua jukumu la matokeo.

"Tulikuwa na mabadiliko mengi katika timu na hii labda ni sababu moja ya uchezaji, lakini ilikuwa muhimu," alisema kocha huyo wa zamani wa Bayern Munich.

„Tulikuwa na mechi nyingi na wachezaji wengi walikuwa wamecheza dakika nyingi sana, ilibidi nichukue tahadhari, hili ni jukumu langu. Ukitaka kumlaumu mtu kwa kipigo hiki, nilaumu mimi.

"Sikuwa na chaguo lingine. Ukiona kwa sasa timu yetu, tuna wachezaji watatu wa kiungo, pamoja na tulikuwa na beki mmoja ambaye ni Eric Garcia katika kiungo.

"Kisha tunaye Marc Casado, tuna Pedri na tuna Pablo Torre. Kwa hiyo, wachezaji wanne. Na unapaswa kufikiria ni wachezaji gani wanaanza. Hili si rahisi lakini tunakubali.

"Baada ya mapumziko ya Oktoba, kuna wachezaji wengi wamerejea, hali tunayo wachezaji wengi waliokuwa majeruhi, lakini hakuna visingizio, inabidi tukubali kushindwa, haikuwa siku yetu bora."



## FIFA yataja viwanja 12 klabu bingwa ya Dunia

**NEW YORK,** MAREKANI




SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa, FIFA, limethibitisha viwanja 12 vitakavyotumika kwenye michuano ya Klabu Bingwa ya Dunia iliyopanuliwa.

Timu 32 kutoka kote ulimwenguni zitasafiri hadi Marekani msimu ujao wa joto kushindana katika shindano lililobadilishwa muundo.

Ulaya itawakilishwa na Klabu 12 - Real Madrid, Chelsea, Manchester City, Bayern Munich, Paris Saint-Germain, Inter Milan, Porto, Benfica, Borussia Dortmund, Juventus, Atletico Madrid na Salzburg.

Wachezaji mashuhuri wamejadili hadharani wazo la kugoma kuhusu idadi ya michezo wanayopaswa kushiriki, huku matatizo ya vifaa yakitishia kuvuruga mipango mizuri ya mashindano hayo.

Lakini juzi FIFA ilishinda kizingiti kikubwa kwa kutangaza viwanja 12 vitakavyoandaa mechi, huku vingi vikiwa kwenye pwani ya mashariki ya Marekani.

Uwanja wa MetLife wa New Jersey, ambao una uwezo wa kuchukua watu 82,500 utakuwa mwenyeji wa fainali ya Kombe la Dunia la FIFA, pia utakuwa mwenyeji wa fainali ya Kombe la Klabu Bingwa.

Uwanja wa Charlotte's Bank of America (74,860), Atlanta's Mercedes-Benz Arena (71,000), Philadelphia's Lincoln Financial Field (69,879), Miami's Hard Rock (64,760) na Orlando's Camping World (60,219) ni viwanja vingine vikuu kwenye pwani ya mashariki, huku eneo la magharibi mwa Pasifiki likishuhudia ‚Rose Bowl' (89,702) na Seattle's Lumen Field (68,740) pia wakiwa wenyeji wa michezo.

Pia kutakuwa na viwanja vinne vya uwezo wa chini vinavyotumika - Uwanja wa Inter&Co huko Orlando (25,500), Geodis Park huko Nashville (30,109), Uwanja wa TQL huko Cincinnati (26,000) na uwanja wa Audi huko Washington DC (20,000).

Rais wa FIFA, Gianni Infantino alisema katika hafla iliyothibitisha viwanja hivyo: "Soka ndio mchezo maarufu zaidi duniani, na mnamo 2025 enzi mpya ya soka ya Klabu itaanza wakati FIFA itakapopanga klabu kubwa zaidi ya kimataifa, inayojumuisha watu wengi zaidi na yenye sifa na ushindani hapa Marekani.

"Shindano la Klabu bingwa ya Dunia 2025 litakuwa na viwanja 12 vya kustaajabisha ambapo sura mpya katika historia ya kimataifa ya soka itaandikwa na wachezaji wakubwa kutoka klabu 32 bora duniani."

Droo ya hatua ya makundi itafanyika Desemba.

HABARI MICHEZO

# AZAM: YATAPITA TU, TUTAREJEA TENA KWENYE KIWANGO CHETU

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kulazimishwa suluhu juzi dhidi ya Mashujaa FC kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, klabu ya Azam FC imesema wanachokutana nacho sasa ni mapito tu na muda si mrefu watarejea kwenye kiwango chao na kuanza kupata matokeo mazuri.

Akizungumza baada ya mchezo huo wa juzi, ofisa habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, alisema Mashujaa waliingia kwa nguvu kwenye mchezo huo hasa baada ya kumbukumbu ya kipigo cha mabao 3-0 ilichokipata kwenye uwanja huo msimu uliopita.

Azam haijapata ushindi kwenye mchezo miwili ya Ligi Kuu, ambapo Alhamisi iliyopita ilishindiliwa mabao 2-0 dhidi ya Simba katika mchezo uliopigwa, Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

"Ni suala la muda tu timu yetu itarudi kwenye kiwango chake, unakumbuka kuwa msimu uliopita tuliwafunga hawa Mashujaa mabao 3-0 hapa hapa, leo walijua nini kingeweza kuwatokea, wakajipanga vizuri na kupata suluhu, na mmeona baada ya mechi walivyokuwa wakishangilia, kama wamepata ushindi, tunajipanga katika mechi ijayo," alisema.

Alibainisha kuwa hakuna kiongozi yeyote wa Azam aliyehuzunika kutokana na matokeo hayo kwani wanajua ni ya kawaida, huku akisema lengo lao la kusaka ubingwa au kusaka nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao ipo pale pale.

Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohamed Abdallah ‚Bares' aliwamwagia sifa wachezaji wake, ingawa alisema kwenye kikosi chake kuna tatizo la kukosa mabao.

"Haikuwa mechi rahisi, niwapongeze vijana wamefanya kazi nzuri licha ya kwamba hatukupata ushindi, tumepata pointi moja inabidi tu tushukuru Mungu, kikubwa tu niseme timu yangu bado ina tatizo la kutotumia nafasi, kwenye mchezo huu tumepata nafasi chache, lakini vilevile tumeshindwa kuzitumia, tungefanya hivyo tungeibuka na ushindi," alisema Bares.

Matokeo ya mechi hiyo yameifanya Azam kushuka kutoka nafasi ya nne hadi nafasi ya tano ikiwa na pointi tisa, ikicheza michezo sita, Mashujaa pamoja na suluhu imeshuka kutoka nafasi ya tano hadi ya sita, pia ikiwa na pointi tisa.




Mchezaji Cyril Brown wa Toyota akijiandaa kupiga mpira kwenye ufunguzi wa mashindano ya gofu ya Airtel jijini Arusha juzi, yaliyoandaliwa na klabu ya Arusha Gymkhana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Songea United yawa tishio 'Championship'

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Songea United, imeanza kuwa tishio kwenye Ligi ya ‚Championship', baada ya juzi kushinda mchezo wake wa pili mfululizo, ikiiadhibu Bigman FC, mabao 2-0, katika mchezo uliochezwa, Uwanja wa Majimaji, mjini Songea, mkoani Ruvuma.

Huu ni ushindi wa pili kwa timu hiyo, katika mchezo wake wa ufunguzi wa ligi hiyo, ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mbeya Kwanza kwenye uwanja huo huo wa nyumbani.

Mabao ya ushindi yalifungwa na nyota wake, Cyprian Kipenye na Ramadhan Kiparamoto.

Kipenye alifunga bao la kwanza dakika ya 66 kwa mkwaju wa penalti, dakika nne baadaye Kiparamoto alipachika bao la pili.

Ushindi huo unaifanya timu hiyo ambayo imebadilishwa jina kutoka FGA Talents iliyokuwa na maskani yake jijini Dodoma, na kuhamia Ruvuma kufikisha pointi sita, huku Bigman, ambayo nayo imebadilishwa jina kutoka Mwadui FC, ikisalia na pointi moja.

Baada ya kukamilika kwa mechi zote nane za raundi ya pili, Mtibwa Sugar inaongoza ikiwa na pointi sita, Songea United nafasi ya pili ikiwa pia na pointi sita, Stand United ya tatu na Biashara United ikiwa nafasi ya nne, zote zikiwa na pointi sita zikitofautiana mabao ya kufunga na kufungwa.

Mchezo mwingine juzi uliochezwa, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, Mbuni FC ikilazimishwa sare ya bao 1-1 na wageni, Geita Gold.

Bao la Mbuni lilifungwa kwa mkwaju wa penalti na Emmanuel Julius, lakini Frank Ikobela aliisawazishia, Geita Gold.

## Gamondi: Si kila mechi tutapata mabao mengi

INATOKA UK. 24

namna tulivyofanya, wachezaji wangu wamejitahidi sana lakini kosa moja tu limewapa nafasi Yanga kupata bao, tunaenda kujipanga kwa ajili ya mchezo ujao," alisema Moalin.

Ushindi huo unaifanya Yanga kufikisha pointi tisa katika michezo mitatu ya Ligi Kuu iliyocheza na kushika nafasi ya nne kwenye msimamo.

## Kocha Fadlu afurahishwa ukomavu wa wachezaji wake vijana

INATOKA UK. 24

kushinda bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji, ikiwa ni siku ya saba.

Alisema katika mchezo wa juzi wachezaji wake walionekana kupata uchovu na ilionekana dakika za mwisho wa mchezo.

"Wachezaji wamepata fatiki, na hili limeonekana dakika za mwishoni mwa mchezo, hatukuwa na shepu nzuri ya kuzuia, mechi tatu kwa wiki ukichanganya na safari ndefu za Libya, Zanzibar na Dodoma zimeonekana kuwaathiri wachezaji wangu, lakini nawapongeza sana kwa sababu wanapambana sana na kupata ushindi licha ya uchanga wao," alisema.

Alisema katika mchezo huo, wachezaji wake kama wangekuwa makini wangeweza kumaliza mechi mapema tu, kwani walipata nafasi nne kipindi cha kwanza.

"Tulianza vizuri tumepata nafasi nne za kufunga, kama tungeweka mpira ndani ya wavu tungekuwa tumemaliza mchezo mapema, tulianza mchezo huu na washambuliaji wawili, tukabadilisha kipindi cha pili, kila kipindi kilikuwa na malengo tofauti," alisema Fadlu.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mecky Maxime, kwa kiasi kikubwa alilia na mwamuzi, Omari Mdoe, akidai hakupaswa kutoa mkwaju wa penalti iliyowapa ushindi Simba kupitia kwa Jean Charles Ahoua.


"Mechi ilikuwa nzuri hata watazamaji wameinjoi, lakini imeamuliwa na makosa ya kibinadamu, sijaona vizuri, lakini nadhani beki wangu kwanza alicheza mpira," alisema.

Ushindi wa Simba, unaifanya kufikisha pointi 12 katika michezo minne iliyocheza na kushinda yote, lakini ikiendelea kusalia nafasi ya tatu huku Dodoma Jiji ikiporomoka nafasi moja kutoka ya tisa hadi ya 10, ikibakia na pointi zake sita baada ya michezo sita.

Michezo
Jumanne Oktoba 1, 2024
Nipashe

## Ten Hag alia na wachezaji wake Man U

UKURASA 21





# Gamondi: Si kila mechi tutapata mabao mengi

**Asema mashabiki lazima wajue kuna kipindi watakutana na matokeo ya…**

Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (katikati), akijaribu kumiliki mpira mbele ya beki wa KMC, Salum Athuman 'Stopper' katika mchezo wao wa Ligi Kuu juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya juzi kushuhudia timu yake ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 na kujikusanya pointi tatu, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hatarajii kuona kila mechi wanapata ushindi wa mabao mengi, lakini kwake muhimu ni pointi tatu.

Kauli ya Gamondi imekuja baada ya baadhi ya mashabiki kuanza kuzungumzia ushindi mdogo wa bao 1-0 walioupata kwenye michezo yao miwili iliyopita ya Ligi Kuu.

Juzi usiku Yanga ilishinda bao hilo moja pekee kwenye mchezo dhidi ya KMC, lakini huo ulitanguliwa na mchezo dhidi ya KenGold FC ambao nao walipata ushindi kama huo na kuanza kuibua maneno kutokana na kawaida ya timu hiyo kupata ushindi mkubwa kwenye michezo yake.

"Sio kila mchezo utapata idadi kubwa ya magoli, ni lazima tucheze kwa kufikiria zaidi pointi tatu, KMC wamecheza vizuri sana, hatujapata mabao mengi lakini nafurahi tumepata pointi tatu, hili ndio jambo la muhimu zaidi," alisema Gamondi.

Alisema kila timu imejiandaa kufanya vizuri na ndio sababu wanapambana uwanjani.

"Itakapotokea kuna nafasi ya kufunga mabao mengi tutakuwa tukifanya hivyo, lakini muhimu sana kupata pointi tatu, hatujafunga mabao mengi kwenye mechi mbili, lakini tumepata pointi zote kwenye kila mchezo," alisema.

Katika mchezo wa juzi usiku uliochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, KMC walijitahidi kuwabana Yanga lakini hata hivyo hawakuwazuia kuondoka na pointi zote tatu.

"KMC wamecheza vizuri sana, walikuwa wengi nyuma ya mpira na hata walipoteza wanarudi wengi golini kwao, wamecheza vizuri na nawapongeza," alisema Gamondi.

Kwa upande wake, Kocha wa KMC, Abdihamid Moalin, aliwapongeza wachezaji wake kwa kufuata maelekezo yake licha ya kuruhusu bao moja lililowapa ushindi Yanga.

"Sio kazi nyepesi kucheza na timu bora kama Yanga ukawabana kwa

INAENDELEA UK. 23

# Kocha Fadlu afurahishwa ukomavu wa wachezaji wake vijana

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Fadlu Davids, ameeleza kufurahishwa na wachezaji wake wengi vijana kwenye kikosi chake ambao hawana uzoefu na michezo mikubwa kumudu kucheza michezo mitatu mikubwa ndani ya siku saba tu na kushinda yote.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo dhidi ya wenyeji, Dodoma Jiji FC, kwenye Uwanja wa Jamhuri mchezo uliomalizika kwa Simba kuibuka na ushindi wa bao 1-0, kocha huyo raia wa Afrika Kusini amesema si rahisi kuwa na kikosi chake kama cha wachezaji wengi vijana ambao hawajawahi kucheza michezo migumu na yenye presha mbele ya maelfu ya mashabiki lakini wakaweza kumudu na kushinda yote.

"Ushindi wa bao moja, pointi tatu, tumeshinda bila kuruhusu bao, hii ni nzuri sana, nadhani tulichofanya hapa ni mwendelezo mzuri, lakini narudia tena kuwa tunacheza michezo hii katika mazingira magumu, tumecheza mechi tatu ndani ya siku saba tu, tena michezo migumu yenye presha kubwa sana ndani na nje ya uwanja kwa mashabiki wetu, tuna wachezaji wengi vijana hawajazoea hili, lakini wameweza kupambana na kuweza kufanya kazi kwa usahihi mpaka kupata ushindi wa asilimia mia moja," alisema Fadlu.

Juzi ilikuwa ni Jumapili ya kwanza tangu Simba ilipocheza mchezo wake wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Barani Afrika dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya, Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikipata ushindi wa mabao 3-1, siku nne baadaye ikacheza mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, Uwanja wa New Amaan Zanzibar, kabla ya siku tatu baadaye, Jumapili iliyopita

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >